# MATUMIZI YA VIFAA VYA KISASA KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA SARUFI: MFANO WA SHULE ZA UPILI ZA KAUNTI NDOGO YA MOIBEN, KENYA

**Melly Kipchirchir Joachim**

**Tasnifu hii imewasilishwa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Elimu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kibabii**

**NOVEMBA, 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO LA MTAHINIWA**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote ile katika chuo chochote kile.

**Melly Kipchirchir Joachim.**

**(MED/KIS/012/15)**

SAHIHI……………………………..… TAREHE ……………………………………

**IDHINI YA WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Kibabii.

Sahihi……………………….. Tarehe ……………………………………….

**Dkt. Misiko Wasike,**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika.

Chuo Kikuu cha Kibabii.

Sahihi ………………………………. Tarehe ……………………….…………………..

**Dkt. Edwin Masinde,**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika.

Chuo Kikuu cha Kibabii.

## IKIRARI NA HATIMILIKI

Mimi, Melly Kipchirchir Joachim nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe, haijawahi kuwasilishwa katika chuo chochote kingine kwa ajili ya shahada kama hii au nyingine yoyote. Tasnifu hii ya Shahada ya Uzamili ya kozi ni kazi inayolindwa kwa mujibu wa makubaliano ya mswada wa kisheria wa Berne, kifungu cha mwaka 1999 na sheria nyingine za kitaifa na kimataifa, kwa niaba ya mwanataaluma. Kazi hii hairuhusiwi kutolewa kwa namna yoyote ile, yote au sehemu, isipokuwa kwa matumizi ya kitaaluma ya utafiti, kujisomea na kurejelea kwa kibali cha maandishi kutoka kwa Mkuu wa Masomo ya Uzamili kwa niaba ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Cleophas Kimeli Birgen na Elizabeth Jeptoo Birgen.

## SHUKRANI

Kazi hii ingawa nimeifanya mwenyewe imechangiwa na watu mbalimbali. Kwanza namshukuru Mola kwa kunipa afya njema na hekima iliyoniongoza katika shughuli hii ya usomi. Mgao wa pili wa shukrani uwaendee wasimamizi wangu Dkt. Misiko Wasike na Dkt. Edwin Masinde kwa kunielekeza katika utafiti wangu ambao kwa hakika ndio sababu ya ufanisi wa kazi hii. Shukrani zangu pia ziwafikie wahadhiri katika Idara ya Kiswahili ya chuo kikuu cha Kibabii kwa mchango wao wa kunihimiza kila mara kujikaza katika masomo haya ya uzamili.

Shukrani zangu vile vile ziwafikie walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Hii ni kwa sababu walikubali kutenga muda wao na kukubali kuhusishwa katika utafiti. Mola awe nanyi na azidi kuwaongoza katika shughuli zenu za ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili. Isitoshe, nawashukuru wanafunzi wa shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben kwa kukubali kuhusishwa katika utafiti.

Haiwezekani kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioanza pamoja masomo haya ya uzamili. Ni vizuri kuwa sote tumekuwa tukisaidiana kuendeleza masomo yetu hadi sasa. Mwisho nawashukuru rafiki zangu wa dhati Victor Kiprop Kigen, John Kiprotich Seurei, Samson Kipkoech Rotich, Titus Serem na Brown Rajwai kwa motisha na changamoto tele ambazo tunatiana mara kwa mara kuhakikisha kuwa tunapiga hatua katika usomi. Nehema zake Mola ziwe nanyi.

**IKISIRI**

Utafiti ulichunguza matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Malengo ya utafiti yalikuwa ni: Kuthibitisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa, kuchunguza jinsi walimu hutumia vifaa vya kisasa katika kufundisha sarufi, kuhakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Utafiti ulifanyika katika kaunti ndogo ya Moiben iliyoko katika kaunti ya Uasin Gishu. Eneo hili lilichaguliwa kimakusudi kuwakilisha maeneo mengine nchini Kenya yenye sifa sawa za ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti uliongozwa na nadharia ya kujifunza kiugunduzi yake Bruner (1966). Utafiti ulizingatia muundo wa utafiti kimfano. Ulilenga shule za upili kumi na tano kati ya ishirini na sita zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben. Walengwa walikuwa walimu kumi na watano wanaofundisha sarufi na wanafunzi mia moja na watano wa kidato cha tatu. Walimu walichaguliwa kwa kuzingatia vipindi vya sarufi ya Kiswahili wanavyovifundisha. Wanafunzi wa kidato cha tatu walihusishwa kwa kuwa mada zilizolengwa katika utafiti zilifundishwa katika kidato cha tatu. Hojaji, mahojiano na uchunzaji zilitumika kukusanya data. Uchunzaji ulitumika kupata data kuhusu vifaa vinavyotumika darasani kufundisha sarufi. Hojaji ya mwalimu na mwanafunzi ilitumika kupata data kuhusu umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Mahojiano yalitumika kupata data kuhusu changamoto za matumizi ya vifaa vya kisasa. Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa kutumia asilimia majedwali. Hatimaye, data hii ilichanganuliwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, chini ya asilimia 20 ya walimu katika kaunti ndogo ya Moiben walitumia tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Matokeo yalithibitisha kuwa, vifaa hivi hurahisisha uelewekaji wa mada za sarufi, huleta uchangamfu darasani, huokoa muda na kuwashirikisha wanafunzi katika somo. Matumizi ya vifaa hivi yanakumbwa na changamoto kama vile: ukosefu wa mtandao shuleni, idadi kubwa ya wanafunzi, hitilafu za umeme, upungufu wa fedha za kuvinunua vifaa hivi, upungufu wa wakati na upungufu wa ujuzi wa matumizi baina ya walimu. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa kwa wizara ya Elimu nchini Kenya. Kutokana na changamoto zinazokumba matumizi ya vifaa vya kisasa, matokeo haya yanaweza yakaisaidia Wizara ya Elimu kubuni mikakati ya kuzikabili changamoto hizi na kuyaboresha matumizi ya vifaa hivi. Aidha, yatawanufaisha walimu wa shule za upili kwa kuwa yatatoa fahamu zaidi kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

**ABSTRACT**

This study, investigated the use of modern teaching and learning aids in teaching and learning of Kiswahili grammar in Moiben sub county of Uasin Gishu county. The research sought: to determine the availability of modern teaching and learning aids, to investigate how teachers use modern teaching and learning aids in teaching and learning of Kiswahili grammar, to evaluate the importance of using modern teaching aids in teaching and learning of Kiswahili grammar. The study was done in Moiben sub county of Uasin Gishu county. This sub county was purposively chosen to represent other sub counties in Kenya with same teaching and learning characteristics. The research was guided by Jerome Bruner's theory of discovery learning. It was a case study in nature. The study was done in 8 schools out of 26 secondary schools in Moiben sub county. Interview schedules, questionaires and observation schedules were used to collect data. Observation schedule was used to observe Kiswahili grammar lessons so as to collect data on the teaching aids used during the lessons. Questionaires were filled by Kiswahili teachers and form three students on the importance of use of modern teaching and learning aids in teaching and learning of Kiswahili grammar. Teachers were interviewed on the challenges they experience while using modern teaching and learning aids in teaching and learning of Kiswahili grammar. Data collected was presented using charts and tables. Findings revealed that less than 20% of teachers in Moiben sub county used modern teaching and learning aids in teaching and learning of Kiswahili grammar. These findings further revealed that use of modern teaching and learning aids is of great importance. The teaching aids made Kiswahili grammar lessons lively, provided easy understanding of grammar, saved on writing time and made the learning process learner centered. It was noted that, teachers in Moiben sub county faced challenges in using computers and laptops connected to projectors. Some of these challenges were: lack of internet in schools, large number of learners, unreliable electricity, lack of funds to purchase modern teaching and learning aids, lack of preparation time, and lack of necessary expertise among teachers in using modern teaching and learning aids. Findings of this research will be of benefit to the Ministry of Education. To curb the challenges facing use of modern teaching and learning aids, the Ministry will come up with mechanisms to improve their usage in secondary schools.

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Hoji-** Kufafanua ukweli wa mambo.

**Shule za Kaunti-** Shule ambazo huwasajili wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka kaunti ambamo shule husika inapatikana.

**Shule za Kaunti ndogo-** Shule ambazo huwasajili wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka Kaunti ndogo ambamo shule husika inapatikana.

**Shule za Kitaifa-** Shule ambazo huwasajili wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka sehemu zote nchini Kenya.

**Shule za viwango vya zaidi ya Kaunti-** Shule ambazo huwasajili wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka kila kaunti.

**Ufundishaji** - Ni tendo la mwalimu kupitisha maarifa kwa mwanafunzi.

**Ujifunzaji** – Ni tendo la mwanafunzi kupokea maarifa kutoka kwa mwalimu.

**Vifaa halisi-** Hivi ni visaidizi vya ufundishaji ambavyo hutumiwa darasani kuhusisha ufundishaji na ujifunzaji na hali halisi maishani kama vile: sarafu, samani, mavazi na mimea.

**Vifaa vya kisasa** – Hivi ni visaidizi vya kielektroniki vinavyohusisha teknolojia mpya ambavyo huweza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji. Hujumuisha tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo.

**Vifaa kongwe** – Hivi ni visaidizi vya ufunddishaji visivyohusisha teknolojia ya kisasa.

**Vyumba vya TEHAMA-** Madarasa maalum yaliyo na vipakatalishi vilivyounganishwa na vinuruweo vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji.

## MAELEZO YA VIFUPISHO

**DFID** - Department for International Development.

**E** – Kielezi

**K.I.C.D** - Kenya Institute of Curriculum Development

**K.I.E** - Kenya Institute of Education.

**KN** – Kundi nomino.

**KT** – Kundi tenzi

**N**- Nomino.

**PDSI** - Plan Do See Improve.

**S**-Sentensi.

**T**- Kitenzi

**TEHAMA**- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**U**-Kiunganishi.

**V**- Kivumishi.

**W**-Kiwakilishi.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI**………………………………………………………………….....….i
**IKIRARI NA HATIMILIKI**……………………………………………………………...iii
**TABARUKU**………………………………………..……………………………………..iv
**SHUKRANI**……………………….……………..……………………………………v
**IKISIRI**………………………………………………………………………………..vi
i
**ABSTRACT**.................................................................................................................... viii
**MAELEZO YA ISTILAHI** ........................................................................................ viiii
**MAELEZO YA VIFUPISHO**……….…………………………………….…………ix
**YALIYOMO**…………………..……………….……………………………….……...x
**SURA YA KWANZA : MISINGI YA UTAFITI**……..…………..……………………………1
1.1 Utangulizi........................................................................................................................ ..1
1.2Usuli wa Utafiti.............................................................................................................. …1
1.3 Suala la Utafiti……………………………………………………….………………..6
1.4 Malengo ya Utafiti… ..................................................................................................... 8
1.5 Maswali ya Utafiti.......................................................................................................... 8
1.6 Sababu za Kuchagua Mada……………………..………………………..……………9
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti………………………………………………………...….9
1.8 Umuhimu wa Utafiti. .................................................................................................... 10
1.9 Nadharia ya Utafiti........................................................................................................ 11
1.10 Hitimisho...................................................................................................................... 16
**SURA YA PILI : UHAKIKI WA MAANDISHI……………………**….…………………….18
2.1 Utangulizi……………………………………………………………….……………18
2.2 Tafiti Kuhusu Mbinu za Ufundishaji wa Sarufi…………………………………………...18
2.3 Tafiti Kuhusu Aina za Vifaa Vinavyotumika katika Ufundishaji na Ujifunzaji. .................. 23
2.4 Tafiti Kuhusu Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Ufundishaji. ...................................... 27
2.5 Tafiti Kuhusu Matumizi Bora ya Vifaa vya Ufundishaji..................................................... 31
2.6 Tafiti Kuhusu Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 34
2.7 Tafiti Kuhusu Changamoto za Matumizi ya Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji…………38
2.8 Hitimisho……………………………………………………………………………43
**SURA YA TATU : MBINU ZA UTAFITI**…………………………………………………...44
3.1 Utangulizi....................................................................................................................... 44

3.2 Muundo wa Utafiti. .......... 44
3.3 Eneo la Utafiti. .......... 44
3.4 Usampulishaji. .......... 45
3.5 Njia za Kukusanyaji Data. .......... 47
3.5.1 Uchunzaji Darasani. .......... 47
3.5.2 Ujazaji wa Hojaji. .......... 48
3.5.3 Mahojiano .......... 49
3.6 Vifaa vya Kukusanya Data. .......... 50
3.6.1 Mwongozo wa Uchunzaji. .......... 50
3.6.2 Hojaji .......... 51
3.6.3 Mwongozo wa Mahojiano. .......... 52
3.7 Utafiti Mwigo. .......... 52
3.8 Unukuzi wa Data. .......... 54
3.9 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data .......... 54
3.10 Maadili ya Utafiti .......... 54
3.11 Matatizo katika Utafiti .......... 56
3.12 Hitimisho .......... 57
**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA** .......... 58
4.1 Utangulizi. .......... 58
4.2 Upatikanaji wa Vifaa vya Ufundishaji kwa Ujumla .......... 58
4.2.2 Upatikanaji wa Vifaa vya Kisasa vya Ufundishaji .......... 61
4.3 Jinsi Vifaa vya Kisasa vya Ufundishaji Vinatumika Kufundisha na Kujifunza Sarufi .......... 63
4.3.1Jinsi Walimu hutumia Tarakilishi Kufundisha. .......... 63
4.3.2 Jinsi Wanafunzi hutumia Tarakilishi Kujifunza .......... 66
4.3.3 Jinsi Walimu hutumia Vipakatalishi Vinapounganishwa na Vinuruweo Kufundisha Vipengele vya Sarufi .......... 68
4.3.4 Jinsi Wanafunzi hutumia Vipakatalishi Vikiunganishwa na Vinuruweo Kujifunza. .......... 74
4.4 Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji wa Sarufi. .......... 75
4.4.1 Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ujifunzaji wa Sarufi .......... 78
4.5 Hitimisho .......... 80
**SURA YA TANO** : **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .......... 81
5.1 Utangulizi. .......... 81
5.2 Muhtasari wa Tasnifu. .......... 81

5.3 Matokeo ya Utafiti. ........................................................................................................ 83
5.3.1 Upatikanaji wa Vifaa vya Kisasa vya Ufundishaji na Ujifunzaji ...................................... 83
5.3.2 Jinsi Vifaa vya Kisasa Vinatumika Kufundisha na Kujifunza Sarufi ................................. 84
5.3.3Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi .. 86
5.4 Hitimisho…………………………………………………………………………......................….88
5.5 Mapendekezo ya Utafiti……………………………………………………….………..…...88
5.6 Mapendekezo ya Tafiti za Baadaye………………………………………………….…...90
**MAREJELEO**. ........................................................................................................................ 91
**KIAMBATISHO A**: **HOJAJI YA MWALIMU**. ....................................................................... 96
**KIAMBATISHO B: HOJAJI YA MWANAFUNZI**............................................................ 101
**KIAMBATISHO C: MWONGOZO WA UCHUNZAJI WA AINA MBALIMBALI ZA VIFAA VINAVYOPATIKANA SHULEN**I......................................................................... 103
**KIAMBATISHO D: MWONGOZO WA UCHUNZAJI WA SOMO LA SARUFI**........... 104
**KIAMBATISHO E: MWONGOZO WA MAHOJIANO**……...………………………...…105
**KIAMBATISHO F: ORODHA YA SHULE ZILIZOHUSISHWA KATIKA UTAFITI**.. 106
**KIAMBATISHO G: RATIBA YA MUDA WA SHUGHULI ZA UTAFITI** ...................... 107
**KIAMBATISHO H: MFANO WA CHUMBA CHA TEHAMA** ........................................ 108
**KIAMBATISHO I: RAMANI YA KAUNTI NDOGO YA MOIBEN**. ............................... 109
**KIAMBATISHO J: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA KIBABII**.................. 110
**KIAMBATISHO K: IDHINI KUTOKA NACOSTI** .......................................................... 111
**KIAMBATISHO L: IDHINI KUTOKA KAUNTI YA UASIN GISHU**……..………...…112
**KIAMBATISHO M: MFANO WA SLAIDI YA UAKIFISHAJI**…………………..…..…113

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imebainisha misingi ya utafiti ambapo imeangazia vipengele vifuatavyo: Usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo, maswali ya utafiti na sababu za kuchagua mada ya utafiti. Vile vile, imedhihirisha upeo na mipaka ya utafiti, umuhimu wa utafiti na nadharia iliyoongoza utafiti huu.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Matumizi ya picha, filamu ya mafunzo na vielelezo vingine katika vita vya pili vya dunia, yalileta mafanikio tele kwa wanajeshi wa Marekani. Johnson (1995), anasema kuwa, baada ya matumizi ya filamu ya mafunzo na vielelezo vingine kutumika katika kuwaandaa wapiganaji wa vita vya pili vya dunia, vielelezo hivi viliendelea kukua na kuenea haswa katika nyanja za elimu kama vile shuleni na katika vyuo vikuu.

Johnson (1995), anasema kuwa, watoto hujifunza bora kwa kuangalia na kuiga tabia za watu wazima. Hii inadhihirisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji utakuwa bora iwapo mwalimu atazingatia stadi za kutazama na kusikiliza. Jambo hili huweza kufanikishwa na matumizi ya vifaa katika ufundishaji. Lengo kuu la kutumia vifaa katika ufundishaji ni, kuinua kiwango au uwezo wa mwalimu wa kuwasilisha somo kwa njia rahisi na inayoeleweka kwa wanafunzi wote. Vifaa huweza kuufanya ufundishaji na ujifunzaji kudumu. Hii ni kwa sababu, mwanafunzi hutumia hisia zaidi ya moja.

Kwa mujibu wa Mdee na wenzake (2014), ufundishaji ni mchakato unaohusisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Mawasiliano huhusisha mwanzilishi wa

ujumbe, njia za kupitisha ujumbe huo na mpokeaji wa ujumbe. Njia za upokeaji wa ujumbe hufanikishwa kwa kuwepo kwa vifaa vya kufundishia.

Kariuki (2017), alilinganisha mawazo haya ya Mdee na wenzake (2014), na mazingira ya darasani. Anasema kuwa, mwalimu kwa wakati mwingi huwa chanzo cha ujumbe naye mwanafunzi huwa mpokeaji wa ujumbe. Anaendelea kusema kuwa, ili mwanafunzi aupokee ujumbe huo kwa njia inayofaa, mwalimu hana budi kutumia vifaa kama kipatanishi kati ya ujumbe unaokusudiwa na mawazo ya mwanafunzi.

Kwa mujibu wa Gathumbi na Ssebbunga (2005), vifaa vya kufundishia lugha ambavyo humwathiri mwanafunzi huwa na sifa zifuatazo: vifaa viweze kuvutia, viweze kuingiliana vizuri na funzo, viweze kukuza umbuji wa mwanafunzi na hatimaye viweze kuingiliana vyema na maisha ya kawaida ya mwanafunzi. Ili kuoanisha matumizi ya vifaa na maisha ya sasa ya mwanafunzi, ni vizuri kwa mwalimu kutumia vifaa vya kisasa katika ufundishaji.

Wringe (1995), alivigawa vifaa vya kufundishia katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile la vifaa vya kimapokezi kama vile vitabu, kadi za maneno, michoro, ubao mweusi, na chaki. Kundi la pili ni lile linalohusisha teknolojia ya kisasa kama vile matumizi ya kinuruweo, tarakilishi na mtandao. Anaendelea kusema kuwa, mgao wa pili unaohusiana na vifaa vya teknolojia ya kisasa ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Swali tunalojiuliza ni je, walimu wa shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben wanazingatia teknolojia ya kisasa katika ufundishaji wao ?.

Zacharia (2012), anashauri kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa vya kufundisha ni nyenzo muhimu sana kwa sababu zinatumika katika ujenzi wa maana katika funzo lolote lile;

zaidi huwa msaada kwa mwalimu katika kurahisisha kazi yake. Utafiti ulitaka kubaini iwapo walimu katika kaunti ndogo ya Moiben wanazingatia ushauri wa Zacharia ( 2012) katika ufundishaji wao wa sarufi ya Kiswahili.

Oldham (2012), anasema kuwa, madhumuni makuu ya kutumia vifaa vya kisasa ni kuinua usomaji wa burudani. Programu za tarakilishi ni mojawapo wa vifaa vinavyoinua hali hii ya usomaji wa burudani. Programu za tarakilishi ambazo huinua usomaji wa burudani zikijumuishwa katika ufundishaji wa Kiswahili huinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Maoni haya ya Oldham (2012), yalichochea utafiti huu kutaka kujua zaidi jinsi walimu wa shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben huhusisha program za tarakilishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Kwa mujibu wa idara ya maendeleo ya kimataifa (Department for International Develop pment, DFID 2009), kuna sifa thabiti ambazo huboresha ufundishaji na ujifunzaji. Mojawapo ya sifa hizi ni vifaa mwafaka vya ufundishaji. Idara hii inaeleza kuwa nchi za Afrika kama vile Malawi na Zimbabwe, zimebuni mikakati maalum ya kuhakikisha kuwa serikali inatoa vitabu vya kiada kwa wanafunzi wa shule za msingi na upili. Katika nchi ya Ethiopia na Uganda, mashirika yasiyo ya kiserikali huwapa wanafunzi vitabu vya kiada.

Mnamo mwaka wa elfu mbili na tisa, nchi ya Tanzania ilianzisha mikakati mipya ya kuinua kiwango cha elimu katika shule za upili. Mikakati hii mipya ilipinga matumizi ya chaki na ubao pekee katika ufundishaji. Kwa mujibu wa (DFID, 2009), ni sharti mwalimu ahusishe vifaa vya kisasa katika ufundishaji. Isitoshe, awahusishe wanafunzi zaidi anapofundisha. Kutokana na mikakati hii wanafunzi wengi nchini Tanzania

wamenufaika. Swali tunalojiuliza ni je, walimu hapa nchini Kenya haswa katika kaunti ndogo ya Moiben wanahusisha vifaa vya kisasa katika ufundishaji wao wa sarufi?

Wambui (2015), katika utafiti wake anasema kuwa, nchini Kenya serikali imepiga hatua katika kuhakikisha kuwa, vifaa vinatumika katika ufundishaji. Kamati ya kitaifa kuhusu ukuzaji na utekelezaji wa mitaala (K.I.C.D 2012), inapendekeza kwamba, vyuo vya ualimu vitenge karakana zao kwa shughuli za kuandaa vifaa vya ufundishaji. Kamati hii, inatambua kuwa mpango bora wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji shuleni ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ya maendeleo ya kielimu. Taasisi hii inaeleza kuwa, ni vigumu kwa mwalimu kufanikisha mafunzo bila kutumia vifaa. Maswali tunayojiuliza ni je, walimu wanatumia vifaa hivi katika ufundishaji na ujifunzaji ?, Je, iwapo wanavitumia, wanahusisha vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji?

Kwa mujibu wa Wambui (2015), ni jukumu la mwalimu kuhakikisha kuwa anatumia vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji ili kutosheleza malengo ya somo lake. Hata baada ya serikali kupitia taasisi mbalimbali za elimu nchini kusisitiza matumizi ya vifaa katika ufundishaji, walimu hawatilii maanani uzito wa matumizi ya vifaa wanapofundisha. Wambui (2015), anasema kuwa, walimu huwa na uvivu katika kuandaa vifaa hivi. Anaendelea kusema kuwa, wahadhiri hawajalipa uzito suala la matumizi ya vifaa katika kuwatayarisha walimu. Walifunzi vile vile hawalipi uzito mafunzo kuhusiana na matumizi ya vifaa katika ufundishaji. Wao huandaa vifaa kwa lengo la kupata alama bora chuoni bali si kujiandaa kwa shughuli za ufundishaji nyanjani. Wambui (2015), anahoji kuwa, hali hii hudhihirika katika mwaka wa tatu wanapokwenda nyanjani. Wengi wao hushindwa kutumia vifaa ipasavyo. Wao huandaa vifaa wakati wa ukaguzi kwa lengo la kumfurahisha mhadhiri anayewatathmini nyanjani na kupata alama.

Walimu wanafaa kuupa uzito unaofaa matumizi ya vifaa wanapofundisha. Hali hii haijadhihirika vizuri katika ufundishaji wa Kiswahili hasusan sarufi. Vifaa vya ufundishaji hutekeleza jukumu kubwa katika kufanikisha ufundishaji wa sarufi. Kama anavyosema Johnson (1995), matumizi ya vifaa huwashirikisha wanafunzi katika hatua zote za ufundishaji na ujifunzaji. Matumizi ya vifaa vya ufundishaji katika kufundisha sarufi huweza kuwapa wanafunzi tajriba thabiti ambayo huwawezesha kujifunza haraka, kuimarisha kumbukumbu na kuelewa dhana kwa urahisi. Hili huimarisha ufundishaji na ujifunzaji na hatimaye kuleta matokeo bora.

Utendaji ni muhimu katika kufundisha na kujifunza. Kufunza kuzuri ni kule kunakosababisha, kusuluhisha na kukuza ujifunzaji. Ili kufanikisha lengo hili, mwalimu hana budi ila kutumia vifaa katika kufundisha. Kujifunza hutokana na mwingiliano kati ya mwalimu, wanafunzi, wazazi na jamii kwa jumla. Matokeo ya ujifunzaji hujitokeza katika mpangilio wa kujifunza unapobuniwa. Matokeo haya hutegemea pakubwa mpangilio uliopo wa shule katika ufundishaji na ujifunzaji. Uelewekaji wa sarufi huweza kutegemea vifaa vya ufundishaji vinavyotumika kurahisisha somo kama wasemavyo Oke na Brown (2006).

Oke na Brown (2006), wanaendelea kusema kuwa, matumizi ya vifaa huweza kuleta mvuto darasani, kuongeza maelezo ya maneno, kuleta uhalisia na kuokoa muda. Kabla ya kuenda nyanjani, walimu huandaliwa ipasavyo vyuoni kuhusiana na matumizi bora ya vifaa katika ufundishaji. Wahadhiri huwaandaa walimu ipasavyo ili kuhusisha mbinu anuwai za ufundishaji nyanjani. Mojawapo ya njia hizi ni njia bora ya matumizi ya vifaa.

Hata hivyo, nafasi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji wa sarufi haijabainika wazi miongoni mwa walimu wa shule za upili. Walimu huhudhuria mazoezi ya kufundisha nyanjani ya lazima kabla ya kufuzu. Wanapojitayarisha chuoni, wao hufundishwa jinsi ya kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia katika ufundishaji. Kutokana na haya, baadhi ya maswali tunayojiuliza ni: Je, walimu huuendeleza ujuzi huu wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji katika kufundisha? Je, wao huhusisha teknolojia ya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia vifaa vya kisasa vya ufundishaji?. Maswali haya na mengine yanatuelekeza kwa suala la utafiti

### 1.3 Suala la Utafiti

Matumizi ya vifaa humsaidia mwalimu kufundisha somo lake kwa ufanisi zaidi na kuwavutia wanafunzi wake katika zoezi zima la kujifunza. Uteuzi bora wa vifaa vya kufundishia humsaidia mwanafunzi kujifunza zaidi kupitia kuona, kugusa, kuonja, kunusa na kusikia. Kutokana na hali hiyo inayomwezesha mwanafunzi kujifunza kikamilifu, mwalimu hana budi kuteua vifaa bora vitakavyomwezesha kuhakikisha mwanafunzi amenufaika na ufundishaji wake. Mwalimu katika shule za kisasa hana budi kutumia nyenzo za kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji badala ya kutegemea tu ubao na vitabu.

Teknolojia mpya kwa sasa imechangamkiwa katika sekta ya Elimu. Serikali ilianzisha mpango wa kuwapa wanafunzi wa chekechea vipakatalishi ili kuinua ufundishaji wa kiteknolojia. Walimu wa shule za upili pia, hawapaswi kuachwa nyuma katika matumizi ya teknolojia mpya wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Miongoni mwa vifaa vya kufunzia vya kiteknolojia ni tarakilishi na vipakatalishi: teknolojia ambayo walimu wa

shule za upili wanastahili kuchangamkia. Matumizi ya vifaa hivi huwawezesha walimu kufanikiwa katika ufundishaji wao kwa vile matumizi yake huwavutia wanafunzi darasani na kuwapa motisha.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji. Masomo ya sarufi yanachosha kwa sababu walimu hutumia mbinu ya mhadhara pekee katika ufundishaji wao. Isitoshe, wanafunzi hupenda masomo ya fasihi kuliko masomo ya sarufi. Hali hii huchangia matokeo yasiyoridhisha katika karatasi ya pili. Matatizo haya huenda ni kutokana na mbinu wanazozitumia walimu. Matumizi ya vifaa vya kisasa huweza kulitatua tatizo hili. Ni katika msingi huu ndipo mtafiti alichagua kutafitia mada ya sarufi ili kuchunguza iwapo matumizi ya teknolojia ya kisasa huweza kuboresha ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi. Isitoshe, mtafiti hajakutana na kazi iliyoangazia matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili. Tafiti ambazo zinakaribiana na utafiti huu zimetafitia matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji wa masomo mengine kama vile Sayansi, Kiingereza, somo la dini na vipengele vya Kiswahili kama vile fasihi simulizi, fasihi andishi na isimu jamii. Kwa hivyo, mtafiti alikwenda nyanjani kuchunguza walimu wanavyofundisha sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa. Wakati huo huo, vyuo vingi vinavyowaandaa walimu vimechangamki teknolojia hii katika maandalizi ya walimu. Mtafiti alichochewa kuenda nyanjani kuchunguza iwapo kuna matumizi ya vifaa hivi vya ufundishaji na ujifunzaji.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Ulidhamiria hususan:

I. Kuthibitisha upatikanaji na aina ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

II. Kuchunguza jinsi walimu na wanafunzi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben hutumia vifaa vya kisasa vya ufundishaji katika kufundisha na kujifunza sarufi

III. Kuhakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji katika kufundisha na kujifunza sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

I. Ni vifaa gani vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben?

II. Walimu na wanafunzi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben hutumiaje vifaa vya kisasa vya ufundishaji katika kufundisha na kujifunza sarufi?

III. Vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji vina umuhimu gani katika kufundisha na kujifunza sarufi?

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti wa Kimani (2015), ulionyesha kuwa, ufundishaji wa sarufi unachosha. Matumizi ya vifaa vya kisasa huweza kuleta uchangamfu darasani. Hii ilimchochea mtafiti kuchunguza matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji wa sarufi. Kwa upande mwingine, Mogeni (2005), anasema kwamba, utumiaji wa vifaa huteka makini ya wanafunzi, huwatia ari na hamu ya kujifunza, huchochea ubunifu wa wanafunzi, hurahisisha maelezo ya maneno, hutoa muhtasari wa yaliyofundishwa na huzindua utaalamu wa wanafunzi. Maoni haya na mengine yalimchochea mtafiti kuchunguza uhalisia wa manufaa ya vifaa vya kisasa nyanjani.

Mtafiti alichagua mada hii kwa kuwa haijatafitiwa. Kutokana na tafiti za awali, ni wazi kuwa watafiti wengi wamechunguza matumizi ya vifaa kongwe katika ufundishaji na ujifunzaji. Ni kwa msingi huu, mtafiti alipata ilhamu ya kutafitia matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

### 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika shule za upili zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben iliyoko katika kaunti Uasin Gishu. Katika kaunti ya Uasin Gishu kuna kaunti ndogo tano. Nazo ni: Moiben, Kapseret, Soy, Kesses na Ainabkoi. Kaunti ndogo ya Moiben ilichaguliwa kwa kuwa shule ya kitaifa ya wasichana ya Moi inapatikana kule. Kwa hivyo, mtafiti alikuwa na uwezo wa kupata data kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa. Utafiti ulihusisha shule kumi na tano katika kaunti ndogo ya Moiben. Shule moja ya kitaifa, shule tatu za kiwango cha zaidi ya kaunti, shule saba za kiwango cha kaunti na shule nne za kiwango cha kaunti ndogo.

Utafiti ulijikita katika taaluma ya ufundishaji na ujifunzaji. Katika taaluma hii kuna mbinu mbali mbali zinazoweza kutumiwa na walimu ili kufanikisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti ulichunguza mbinu ya ufundishaji kwa mujibu wa vifaa vya kisasa.

Vifaa mahususi ambavyo utafiti ulilenga ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo. Hii ni kutokana na mabadiliko katika mbinu za kufundishia yanayohitaji mbinu za kisasa ili kuleta matokeo mazuri. Katika kuchunguza matumizi ya vifaa vya kisasa, utafiti ulijikita katika kipengele cha sarufi wala si lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

Kipengele cha sarufi kilichaguliwa kwa vile tafiti za awali zilionyesha kuwa wanafunzi hawafurahii vipindi vya sarufi. Kimani (2015), anahoji kuwa, hali hii husababisha matokeo yasiyoridhisha katika mtihani wa kidato cha nne. Katika kuchunguza ufundishaji wa sarufi katika shule za sekondari, utafiti ulilenga mada za sarufi zinazofundishwa katika kidato cha tatu. Utafiti ulilenga kidato cha tatu kwa kuwa, mada hizo hazifundishwi kwa kina katika kidato cha kwanza na kidato cha pili ilhali wanafunzi wa kidato cha nne wanajitayarisha kwa mtihani wa kitaifa.

### 1.8 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yalitoa taswira ya matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Vifaa hivi vya kisasa ni : matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo. Kadri ulimwengu unavyozidi kubadilika, ndivyo mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazidi kubadilika. Kwa hivyo, utafiti huu unatoa mwanga kuhusu matumizi haya ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Utafiti huu unatoa mapendekezo kuhusu uboreshaji wa ufundishaji kwa kutumia vifaa

vya kisasa katika kufundisha na kujifunza sarufi ili kuyainua zaidi matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili.

Utafiti huu vile vile ni mchango kwa tafiti zilizofanywa kuhusu matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Unatoa mchango haswa kuhusu matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Matokeo ya utafiti huu yanawafaa washikadau wengi katika sekta ya elimu. Washikadau hawa ni walimu wanaofundisha Kiswahili, wanafunzi na wakuza mitalaa. Walimu wanaofundisha Kiswahili ndio wateuzi na watumizi wa vifaa. Kwa hivyo, hawana budi kuingiza usasa katika uteuzi na utumizi wao wa vifaa vya kufundishia. Wanafunzi walinufaika kwa kuwa walishirikishwa katika matumizi haya ya vifaa vya kisasa katika ujifunzaji wa sarufi.

Wakuza mitalaa wanatarajiwa kutoa mwelekeo kuhusu vifaa vinavyofaa kutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, ilibainika kuwa mwelekeo bora ni ule unaohusisha matumizi ya vifaa vya kisasa hasa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo. Utafiti huu vile vile unatarajiwa kuchochea tafiti zaidi katika uwanja huu mpana wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 1.9 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ujifunzaji kiugunduzi yake Bruner (1966). Nadharia ya ujifunzaji kiugunduzi, hushikilia kuwa, ni vizuri kwa wanafunzi kujifunza kwa kuhusisha kile kinachofundishwa na mazingira ya hali halisi. Matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji huweza kuleta uhalisia na hivyo kuwaongoza wanafunzi

kuvumbua wenyewe na kurahisisha uelewekaji wa sarufi kwa haraka. Utafiti ulifanywa huku ikitiliwa maanani kuwa vifaa vya aina mbali mbali vikitumiwa kwa njia inayofaa, huweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari. Bruner (1966), alitilia mkazo nafasi ya mazingira na tajriba katika kukuza uwezo wa kiakili. Kwa kuwa alikuwa na shauku ya kuchunguza lugha na uwasilishaji wa mawazo ya binadamu, Bruner (1966), alichunguza maendeleo ya kiugunduzi katika lugha ya watoto. Kutokana na uchunguzi wake, Bruner (1966), alipendekeza kuwa, kwanza mwanafunzi anafaa kuwa mshiriki katika kila mchakato tendi ambao wanafunzi huibua na kubuni dhana mpya zilizo na msingi kwenye yale wayafanyayo. Anaendelea kusema kuwa, mwanafunzi huteua dhana alizojifunza na kuzigeuza au kuzitumia kupata maarifa mpya. Aidha Bruner (1990), anazidi kusisitiza kuwa, shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji ni shughuli hai ambao huhitaji ushiriki wa mwanafunzi katika hatua zote za ujifunzaji.

Nadharia hii ina mihimili mitano ambayo ni:

I. Muundo bora wa ufundishaji na ujifunzaji. Katika mhimili huu, ufundishaji unafaa kuwa wa kidayolojia baina ya mwalimu na mwanafunzi. Mwanafunzi anafaa kuchukuliwa kama mhusika anayeshiriki kwa upana katika ufundishaji na ujifunzaji. Krashen (1988), anakubaliana na maoni haya ya Bruner (1966), anaposema kuwa, mbinu bora za ufundishaji ni zile zinazotilia maanani ushiriki mpana wa mwanafunzi anayeelekezwa na mwalimu. Kulingana na Krashen (1988), ufundishaji na ujifunzaji unaokuza uwezo wa ugunduzi ni matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji

II. Maandalizi kabla ya kuwasilisha somo ni muhimu katika kufanikisha ubora wa somo. Kwa mujibu wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi, lengo kuu la ufundishaji na

ujifunzaji ni kumpa mwanafunzi fursa ya kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji wala si kumwezesha tu mwanafunzi kupata dhana katika akili yake. Hill (1999), alihusisha nadharia hii ya kujifunza kwa ugunduzi na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Anasema kuwa, mbinu bora ya kufundisha inayohusisha mwanafunzi katika hatua zote ni ile inayotumia vifaa vya kufundishia. Hill (1999), anashikilia kuwa, matumizi ya vifaa vya ufundishaji humpa mwanafunzi fursa ya kuwa mshiriki mkuu katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. Anawashauri walimu kuhusisha matumizi ya vifaa katika maandalizi ya masomo yao.

III. Mwanafunzi hupata maarifa zaidi kwa kutazama. Mhimili huu unashikilia kuwa, kwa ujumla, ujifunzaji ni matokeo ya mwanafunzi kuhusisha maarifa aliyoyapata kwa hali na miktadha mipya anayokumbana nayo maishani. Bruner (1966), anasema kuwa, ili mwanafunzi aweze kukumbuka dhana anazofundishwa, hana budi kupewa majukumu ya kushiriki katika upataji wa dhana hizo. Anatilia mkazo nafasi ya mwalimu katika kubuni mazingira ambamo ujifunzaji hutokea na vile vile kumsaidia mwanafunzi kung'amua yale asiyoweza kufahamu kwa juhudi za kibinafsi.

IV. Ari ya mwanafunzi ya kutaka kujua zaidi inafaa kuchochewa na mwalimu. Nadharia hii inaeleza kuwa, ili ujifunzaji upatikane, lazima kuwe na maingiliano kati ya funzo na mwanafunzi. Hapa matumizi ya vifaa katika ufundishaji hufanikisha maingiliano hayo. Katika kiwango hiki, matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji humsaidia mwalimu kutoa mwelekeo zaidi ili kulifanya somo lake lieleweke kwa urahisi.

V. Mwalimu anapaswa kuanza na mambo rahisi yanayofahamika kwa wanafunzi wote huku akielekea kwa mambo magumu. Katika mhimili huu, ufundishaji unafaa kuanza kwa kurejelea wanachokifahamu wanafunzi na kuelekea kwa kile wasichokifahamu.

> Hapa wanafunzi huingia darasani wakiwa tayari na tajriba na maarifa fulani ambayo yanaweza kuwafanya kuelewa wanachofundishwa. Ufundishaji mzuri ni ule unaorejelea maarifa na tajriba hizo. Hill (1999), anahoji kuwa, matumizi ya vifaa vya ufundishaji huwapa wanafunzi nafasi nzuri ya kutagusuna na tajriba hizi hivyo basi kuufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa rahisi.

Marzano (2011), akichangia kuhusu nadharia ya Bruner (1999), anasema kuwa, nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi imebainisha kuwa ufundishaji ni mchakato ambao huhusisha kumtayarisha mwanafunzi kugundua mambo mwenyewe kwa kutazama au kisikia. Anaendelea kusema kuwa, kazi ya mwalimu ni kumwongoza mwanafunzi kwa kumpa maarifa yanayohitajika na kumwacha mwanafunzi kugundua mwenyewe. Uongozi huu wa mwalimu kwa mwanafunzi huhitaji maagizo ya moja kwa moja.

Vile vile, Roya na Hanieh (2015), walichangia katika kuiboresha nadharia hii. Wanahoji kuwa, nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi husisitiza jinsi wanafunzi wanafaa kuvitumia vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kujifunza kwa njia bora zaidi. Wanazidi kuhoji kuwa, walimu wanafaa kutilia mkazo kile ambacho wanafunzi wanakifahamu na kuwapa fursa ya kuyaweka maarifa haya katika mazoezi. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, ufundishaji na ujifunzaji unapaswa kuwa shughuli hai. Wanafunzi wanafaa kushirikishwa ipasavyo. Wanahoji kuwa, ufundishaji na ujifunzaji unafaa kuhusisha hali halisi. Hali hii itamwezesha mwanafunzi kuelewa dhana kwa njia bora zaidi. Kwa mujibu wa Roya na Hanieh (2015), uhusishaji wa teknolojia ya kisasa katika ufundishaji huwashirikisha wanafunzi katika hatua zote za ujifunzaji. Hali hii huwapa wanafunzi motisha ya kufunza kwa njia bora zaidi.

Wakimnukuu Hare (2005), Roya na Hanieh (2015), wanahoji kuwa maelekezo ya nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi yanafaa kutiliwa maanani katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Hare (2005), anasisitiza kuwa, shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji inafaa kuwashirikisha wanafunzi katika hatua zote. Kwa mujibu wa Hare (2005) uhusishaji wa teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji ni mbinu bora ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki ipasavyo katika somo. Akishadidia maelekezo ya Bruner (1966), Christie (2005), anahoji kuwa, mbinu bora ya ufundishaji na ujifunzaji ni ile ambayo inampa mwanafunzi fursa ya kugundua mambo mwenyewe.

Nadharia hii inasisitiza kuwa, wanafunzi wanafaa kushirikishwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Bruner (1966), anaeleza kuwa, ufundishaji si kuhamisha maarifa tu kutoka kwa mwalimu hadi kwa mwanafunzi bali huhusisha jinsi mwanafunzi anashirikishwa katika mchakato huu. Bruner (1966), anazidi kuhoji kuwa, wanafunzi huingiliana na mazingira kwa kuchunguza na kutazama. Kwa hivyo, matumizi ya vifaa vya kisasa huweza kuleta athari hiyo ya kutazama na kuchunguza.

Kwa mujibu wa Bruner (1966), sifa kuu ya ufundishaji kwa ugunduzi, inahusu jinsi ambavyo watu hupata maarifa kutokana na matukio ya awali. Alisisitiza kuwa, sifa kuu ya ufundishaji wa kiugunduzi ni kumhusisha mwanafunzi na kumpa kipaumbele katika hatua zote za ufundishaji na ujifunzaji. Matumizi ya vifaa huweza kutekeleza jambo hili. Huo ndio msingi uliochangia katika uteuzi wa nadharia hii kutafitia matumizi ya vifaa vya kufundishia sarufi katika shule za sekondari.

Nadharia hii vile vile inasisitiza kwamba, katika ufundishaji, njia mwafaka inafaa kutiliwa maanani kuliko kusisitiza matokeo. Matumizi ya vifaa vya kisasa katika

ufundishaji na ujifunzaji huweza kuwa njia mwafaka ya kufundishia na kujifunzia sarufi. Utafiti huu ulinuia kuweka wazi wazo hili. Utafiti huu ulitumia mihimili mitatu ifuatayo:

I. Muundo bora wa ufundishaji na ujifunzaji. Hapa, muundo unaotumika katika kuwasilisha somo ndio unaotiliwa maanani na wala si kuwapa tu maarifa wanafunzi. Utafiti ulilenga kutathmini iwapo matumizi ya vifaa vya kisasa vya kufundishia huweza kuwa muundo bora wa kufundisha.

II. Mwanafunzi kupata maarifa zaidi kwa kutazama badala ya kuambiwa na mwalimu. Utafiti ulilenga kuthibitisha iwapo vifaa vya kisasa vya kufundishia vya kutazama, ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo, vinatumika katika kufundisha sarufi na athari ya kupata maarifa zaidi kwa kutazama inavyoweza kujitokeza.

III. Ari ya mwanafunzi ya kutaka kujua zaidi kuchochewa na mwalimu. Mwalimu ana jukumu la kutekeleza kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata hamu ya kujifunza. Utafiti ulilenga kubaini iwapo matumizi ya vifaa vya kisasa huweza kuteka ari ya wanafunzi ya kutaka kujifunza.

Kwa ujumla utafiti ulitumia mihimili mitatu kati ya mitano. Mihimili iliyotumika ilikuwa: mhimili wa kwanza, wa tatu na wa nne.

### 1.10 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia usuli wa mada ya utafiti. Suala la utafiti vile vile limeangaziwa. Aidha, malengo na maswali ya utafiti pia yameshughulikiwa. Isitoshe, Sababu za uchaguzi wa mada hii pia zimedhihirishwa. Katika upeo na mipaka, utafiti ulijikita katika taaluma ya ufundishaji na ujifunzaji. Ulilenga kipengele mahususi cha sarufi. Umuhimu

wa utafiti vile vile umezungumziwa katika sura hii. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ambayo ni nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi yake Bruner (1966), vile vile imeangaziwa kwa kina katika sehemu hii. Sura inayofuata imeshughulikia tahakiki ya maandishi.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia imetoa msingi wa utafiti kwa kuangazia masuala mbalimbali. Miongoni mwa yale ambayo yamezungumziwa ni usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, umuhimu wa utafiti na nadharia iliyoongoza utafiti huu. Sura hii imeshughulikia tahakiki ya maandishi. Uhakiki huu wa maandishi ulifanyika kwa kuzingatia mada ya utafiti. Uhakiki ulihusu mbinu za ufundishaji wa sarufi, aina za vifaa vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji na umuhimu wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji. Vile vile, ulihakiki matumizi bora ya vifaa vya ufundishaji, matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji. Hatimaye, changamoto zinazokumba matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji zilihakikiwa.

## 2.2 Tafiti Kuhusu Mbinu za Ufundishaji wa Sarufi

Njoroge (2014), anahoji kuwa, nyimbo huwasaidia wanafunzi kuelewa dhana haraka. Nyimbo huwa muhimu katika kufundisha nyakati na hali, ukanushaji na vinyume vya vitenzi. Njoroge (2014) aligundua kuwa, wanafunzi hupata changamoto tele katika kipengele cha sarufi. Anawashauri walimu kuhusisha mbinu bunifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Matokeo ya utafiti wa Njoroge (2014), yalithibitisha kuwa, nyimbo ambazo ni fupi, zenye kueleweka, zilizo rahisi kukumbuka na zenye kutumbuiza husaidia katika ufundishaji wa msamiati, nyakati na hali na ukanushaji. Matumizi ya nyimbo huteka makini ya wanafunzi, huleta uchangamfu na kuleta uvutio katika somo la sarufi. Njoroge (2014), anasema kuwa, ili kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa

sarufi, mwalimu hana budi kuhusisha mbinu bunifu katika ufundishaji wake. Matumizi ya vifaa vya kisasa ni mbinu bunifu ya kufundisha na kujifunza sarufi. Mtafiti alilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Naye Githinji (2017), anasema kuwa, ukosefu wa matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi ni jambo kuu linalochangia matokeo mabaya ya wanafunzi katika somo la Kiswahili katika shule za sekondari zilizoko Baringo ya kati. Ilidhihirika kuwa, kulikuwa na uhaba wa walimu waliofuzu kufundisha Kiswahili. Hata hivyo, Githinji (2017) anahoji kuwa, walimu wana mtazamo chanya kuhusu matumizi ya vifaa vya kufundisha na kujifunza. Ilibainika kuwa walimu walitumia mbinu ya mhadhara pekee katika kufundisha sarufi. Hali hii ilichangia pakubwa matokeo mabaya ya ufundishaji wa sarufi.

Kwa mujibu wa Githinji (2017), wanafunzi zaidi ya asilimia 80% walikiri kupenda masomo ya fasihi kuliko masomo ya sarufi. Hali hii ilichangia matokeo yasiyoridhisha katika karatasi ya pili. Githinji (2017), alitafitia kipengele cha sarufi kama ulivyo utafiti huu. Hata hivyo, tofauti ni kuwa, mtafiti alilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben huku Githinji (2017) akilenga matumizi ya vifaa kongwe vya ufunzaji na ujifunzaji.

Kwa mujibu wa utafiti wa Ogero (2012), matokeo katika karatasi ya pili hayakuwa ya kuridhisha ikilinganishwa na karatasi ya kwanza na karatasi ya tatu. Hali hii ilichangia matokeo ya Kiswahili kwa jumla kuwa duni. Ogero (2012), anasema kwamba, walimu

hawakutumia mbinu bora za ufundishaji. Mbinu ya mhadhara pekee ilitumika. Asilimia 70% ya walimu katika kaunti ndogo ya Sameta walikiri kutumia mbinu ya mhadhara kufundisha sarufi. Utafiti wa Ogero (2012), ulithibitisha kuwa, vitabu vya kiada vilitumika kama vifaa vikuu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Utafiti wa Ogero (2012), ulihusu ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama ulivyo utafiti huu. Hata hivyo, tofauti ni kuwa utafiti huu ulilenga kipengele cha sarufi ilhali utafiti wa Ogero (2012), ulilenga Kiswahili kwa jumla. Vile vile, utafiti wangu ulilenga mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo.

Kulingana na King’ei (2007), sheng imeenea sana miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya. Kuenea kwa sheng kumeathiri ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kwani wanafunzi wa sekondari wanakiuka sheria za sarufi katika mazungumzo. Ilibainika kuwa, tatizo hili lina athari hasi katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Kingei (2007), anasema kuwa, ili kukabiliana na makali ya sheng, walimu wanafaa kutilia maanani ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Kwa kufanya hivi, walimu wanafaa kutumia mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji ili kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Matumizi ya vifaa vya kisasa ni mbinu bora ya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Mbinu hii huboresha ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi na hivyo kupunguza makali ya sheng . Hii ni kwa sababu mbinu hii huwapa wanafunzi msingi bora wa sarufi na matumizi ya lugha. Utafiti huu ulilenga kutathmini matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika

pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Kwa mujibu wa Ambuko (2013), matumizi ya nyenzo ni mbinu bora ya ufundishaji na ujifunzaji. Hata hivyo, Ambuko (2013) alithibitisha kwamba, nyenzo zilitumika kufundisha fasihi pekee. Nyenzo hazikutumika kufundisha sarufi. Anaendelea kuhoji kuwa, asilimia 80% ya walimu walitumia mbinu ya mhadhara kama mbinu kuu ya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Isitoshe, ubao na chaki pekee zilitumika kama vifaa kuu vya kufundishia.

Utafiti wa Ambuko (2013), ulilenga mbinu ya ufundishaji wa Kiswahili jumla kwa kutumia vifaa kongwe. Utafiti huu ni tofauti na wa Ambuko (2013) kwa kuwa wangu ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo katika kufundisha na kujifunza sarufi pekee wala si lugha ya Kiswahili kwa jumla.

Naye Magare (2017), anasema kuwa, majadiliano ya vikundi yanaimarisha uelewekaji wa sarufi kwa kuwa wanafunzi wanahusishwa zaidi katika ujifunzaji. Matokeo ya utafiti wake yalithibitisha kuwa ukosefu wa muda ni changamoto kuu katika matumizi ya majadiliano ya vikundi. Utafiti wa Magare (2017), ulichunguza kipengele cha sarufi. Hata hivyo, tofauti ni kuwa utafiti wa Magare (2017), alitafitia mbinu ya majadiliano ya vikundi ilhali utafiti huu ulilenga mbinu ya kufundisha kwa kutumia vifaa vya kisasa vya ufundishaji ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo katika kufundisha na kujifunza sarufi katika shule za sekondari zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Achila (2010), alitafitia matumizi ya mbinu ya kimuktadha katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati wa Kiswahili katika shule za upili za wilaya ya Kakamega. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa, walimu hawakutumia mbinu ya kimuktadha katika ufundishaji wa msamiati. Ilibainika kuwa walitumia mbinu nyinginezo kufundisha msamiati. Mbinu ya mhadhara ilitumika zaidi. Vile vile, walimu walihusisha chati kama kifaa kikuu cha ufundishaji.

Utafiti wa Achila (2010), ulilenga msamiati ambacho ni kipengele cha sarufi. Vile vile, ulihusu mbinu ya ufundishaji. Hata hivyo, kinyume na utafiti wa Achila (2010), utafiti huu ulilenga mbinu ya ufundishaji wa sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Naye Onwonga (2014), aligundua kuwa, matumizi ya vifaa vya ufundishaji huwa muhimu kwa walimu na wanafunzi. Anahoji kuwa, matumizi ya vifaa hivi hurahisisha uwasilishaji wa somo la sarufi darasani. Matokeo yaliendela kubaini kuwa, walimu walitumia vifaa katika kufundisha sarufi ya Kiingereza japo kwa viwango vya chini mno. Hata hivyo, Onwonga (2014), anakubali kuwa, vifaa vya kufundishia hurahisisha uelewekaji wa somo la sarufi. Utafiti wa Onwonga (2014), ulilenga matumizi ya vifaa vya kufundishia sarufi ya Kiingereza kinyume na utafiti huu ambao ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa katika kufundisha na kujifunza sarufi ya Kiswahili.

Okwako (1994), akithibitisha umuhimu wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji, anahoji kuwa, vitabu vya kiada na vya ziada ni muhimu sana kwani humpa nafasi mwanafunzi kusoma kwa mapana. Isitoshe, humpa mwanafunzi nafasi ya kufanya utafiti zaidi. Utafiti

wa Okwako (1994), ulilenga matumizi ya vitabu vya kiada kama mbinu mojawapo ya kufundisha na kujifunza sarufi katika shule za upili kinyume utafiti huu ambao ulichunguza mbinu ya ufundishaji wa sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

**2.3 Tafiti Kuhusu Aina za Vifaa Vinavyotumika Katika Ufundishaji na Ujifunzaji**

K.I.E (2006), imevigawa vifaa katika makundi matatu makuu: vifaa vya kusikilizwa, kutazamwa na vile vya kutazamwa na kusikilizwa. Vifaa vya kusikilizwa huimarisha mafunzo kupitia kwa kusikilizwa. Vifaa vya kutazamwa huimarisha ufundishaji na ujifunzaji kupitia kwa kutazamwa na vya kutazamwa na kusikilizwa huimarisha mafunzo kupitia kwa kusikia sauti na kutazama picha na michoro. Mifano ya vifaa vya kusikia ni kama vile: kanda za sauti, redio, tarakilishi, filamu na tepurekoda. Navyo vifaa vya kutazamwa ni kama vile: vibonzo, ubao, michoro, picha, vifaa halisi, magazeti na vinyago. Vifaa vya kutazamwa na kusikiliza ni kama vile: filamu, televisheni, wanasarakasi, wageni waalikwa, video na tarakilishi.

Uainisho huu wa vifaa ni muhimu kwa sababu uliusaidia utafiti huu katika kutambua migao mikuu ya vifaa vya kisasa vinavyotumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule mbalimbali za sekondari. Utafiti huu ulilenga mgao wa tatu ambao ni matumizi ya vifaa vya kisasa vya kutazamwa na kusikilizwa haswa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben.

Taasisi ya elimu ya (K.I.E) ingali inatoa mafunzo kwa kutumia redio kupitia kwa Shirika la Utangazaji la Kenya (K.B.C). Taasisi hii huzipa shule zote nchini ratiba inayoonyesha wakati wa kufunzwa kwa somo la Kiswahili katika muhula husika. Odera (2007), alitafitia ufaafu wa vipindi vya Redio katika kufundisha Kiswahili. Kwa mujibu Odera (2007), vipindi hivi huwapa wanafunzi fursa ya kufunzwa na walimu tofauti ambao pia ni wataalamu katika somo husika. Kufunzwa na walimu tofauti huleta uchangamfu darasani na kuwapa wanafunzi ari ya kujifunza. Odera (2007), alitafitia matumizi ya kifaa cha kisasa ambacho ni Redio kinyume na utafiti huu ambao ulilenga matumizi ya vifaa mahususi vya kisasa vya ufundishaji ambavyo ni tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo. Odera (2007), alitafitia ufundishaji wa Kiswahili kwa jumla ilhali utafiti wangu ulilenga kipengele cha sarufi pekee.

Naye Ornstein (1990), anataja aina za vifaa kama vile filamu, tarakilishi na video kama vifaa muhimu katika ufundishaji. Anasema kuwa, vifaa hivi huimarishana na kufidiana. Anaendelea kusema kuwa, si vyema kumhukumu mwalimu anayetumia kifaa kimoja mahali pa nyingine isipokuwa ni bora mwalimu kutumia vifaa mbalimbali wala asitegemee kifaa kimoja tu kwani huenda ikawachosha wanafunzi au kuchukuliwa kama kitu cha kawaida tu.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi walimu katika kaunti ndogo ya Moiben hushirikisha matumizi ya vipakatalishi kinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Uainishaji huu wa Ornstein (1990), ulifaa utafiti huu kwa kuwa ulihusisha matumizi ya tarakilishi kama kifaa muhimu katika kufundisha na kujifunza. Utafiti wangu ulilenga kuchunguza matumizi haya ya tarakilishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben.

Akishadidia maoni ya Ornstein (1990), Walker (1999), anataja filamu kama kifaa chenye ushawishi na mvuto wa hali ya juu ikitumika katika ufundishaji. Filamu huweza kutumika kufanikisha mafunzo kuhusu msamiati. Filamu huwa ni za bei nafuu na ni rahisi kuhifadhi na kutumia. Maoni haya ya Walker (1999), yanathibitisha kwamba pana haja ya kuhusisha teknolojia ya kisasa katika ufundishaji. Hii ni kwa sababu, filamu ni aina mojawapo ya vifaa vya kisasa vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji.

Hata hivyo, Walker (1999), alitaja kifaa kimoja pekee cha ufundishaji ambayo ni filamu. Utafiti huu ulilenga matumizi ya vifaa vitatu vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji ambavyo ni tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben.

Kwa upande mwingine, Dorr (1984), anaeleza kuhusu televisheni kama kifaa muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Anaeleza kuwa, televisheni ni kifaa muhimu kwa kuwa ina mvuto kwa wanafunzi. Televisheni huwa na vipindi vya kielimu ambavyo huelimisha umma kwa jumla na kuna vipindi vya mafunzo ambavyo huandaliwa na wizara ili kufikia shule na vyuo. Naye Oginga (2010), anataja televisheni kama chombo ambacho kinaweza kufikia watu wengi na ni chombo cha kimsingi cha elimu. Vipindi vya televisheni si rahisi kuja kwa wakati unaofaa isipokuwa kama ni vipindi vinavyotayarishwa na idara ya elimu au vile ambavyo vinaandaliwa shuleni. Ingawa kuunda mifumo hii ni ghali sana walimu wanaweza kunakili vipindi vya televisheni kwenye kanda na kuvitumia baadaye.

Maoni ya Dorr (1984) na Oginga (2010), yanathibitisha kuwa, televisheni ni kifaa cha kisasa ambacho kinaweza kutumiwa katika ufundishaji kama yalivyo matumizi ya

tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo. Utafiti wangu ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo ni tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben kinyume na utafiti wa Oginga (2010) ambao ulilenga matumizi ya televisheni.

Hatimaye, Papert (1987), anataja matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha ufundishaji. Anasema kuwa, tarakilishi huweza kutekeleza majukumu mengi ya kielimu. Tarakilishi hutumika bora pamoja na vifaa vingine kama vile printa na vinuruweo. Vifaa hivi humruhusu mwalimu na mwanafunzi kuchagua vipindi bora kwa mafunzo yao. Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kinyume na wa Papert( 1987), ambao ulilenga matumizi ya tarakilishi kwa ujumla katika ufundishaji.

**2.4 Tafiti Kuhusu Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Ufundishaji**

Kwa mujibu wa Too (1996), matumizi ya vifaa katika ufundishaji wa hesabu huwa muhimu sana. Anasema kuwa, vifaa huwashirikisha wanafunzi katika hatua zote za ufundishaji, hurahisisha ufahamu wa wanafunzi kwa kuwa wanafunzi hujifunza kwa kutenda, huwawezesha kuwa na kumbukumbu ya muda mrefu na kuwachangamsha wanafunzi kwa kuwapa ari ya kutaka kujifunza zaidi. Utafiti wa Too (1996), ulilenga matumizi ya vifaa katika shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji.

Hata hivyo, ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa ulilenga ufundishaji wa hesabu ilhali utafiti wangu ulilenga kipengele cha sarufi katika lugha ya Kiswahili. Isitoshe, utafiti wa Too (1996), ulilenga vifaa vyote vya ufundishaji na ujifunzaji kwa jumla katika

kufundisha na kujifunza hesabu ilhali utafiti huu ulilenga matumizi ya vifaa mahususi vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben.

Wakati huo huo, Koross na Murunga (2017), wanasema kwamba vifaa vya ufundishaji humotisha ufundishaji kwa kuwa zitumiwapo, mwanafunzi huelewa na kukumbuka funzo kwa muda mrefu. Kuna msemo maarufu wenye hekima kutoka Uchina uliodahiliwa na mwanafilosofia Confucius kuwa: *nisikiacho, hukisahau, nikionacho, hukikumbuka na nikitendacho, hukibwia milele.* Kwa mujibu wa wanasaikolojia, binadamu hujifunza asilimia kumi (10%) kupitia mlango wa kusoma na asilimia ishirini (20%) kwa mlango wa kusikia. Anaweza kuhifadhi asilimia hamsini (50%) ya yote anayojifunza kwa kuona na kusikia na asilimia sabini (70%) kwa kuandika na kusema na asilimia tisini (90%) kwa kutenda na kusema.

Kutokana na madai haya ya wanasaikolojia, mwanafunzi anahitaji kutumia vifaa atakavyoviona na kushika iwapo atatarajiwa kutekeleza mambo kikamilifu na kuyashika mafunzo kwa wakati ufaao. Kwa kuzingatia maelezo haya ya koross na Murunga (2017), utafiti huu ulilenga kuhakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji ambavyo ni: matumizi tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Kwa upande mwingine, Eshiwani (1988), anahoji kuwa, walimu na wanafunzi hawapati matokeo bora kwa sababu hawatumii vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Eshiwani (1988), anasema kwamba, matumizi ya vitabu vya kiada ni muhimu sana kwani husaidia

kumbukumbu ya yale yaliyofundishwa. Isitoshe, huwapa wanafunzi fursa ya kufanya marudio kwa mapana bila mwalimu. Matokeo ya utafiti wa Eshiwani (1988), yaliendelea kubaini kuwa vifaa vya ufundishaji vikitumika ipasavyo, huwachangamsha wanafunzi na kulifanya somo liwe hai. Utafiti wa Eshiwani (1988), ulilenga matumizi ya vifaa vya ufundishaji. Hata hivyo, alilenga matumizi ya vitabu vya kiada pekee kinyume na utafiti huu ambao ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Akishadidia maoni ya Eshiwani (1988), Quist (2006), anasema kuwa, vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji huwatia wanafunzi motisha, huchangia uelewekaji, hutoa tajriba tofauti, huongeza msisitizo kwa mafunzo, huhimiza uhusikaji na hubadilisha mitazamo. Utafiti huu ulilenga kuhakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben.

Naye Skinner (2003), anasema kuwa, mwalimu anastahili kuwa mtaalamu anayetekeleza majukumu yake kitaalamu na anayetoa maamuzi bora katika kazi yake. Lazima aelewe kuhusu hisia za mwanafunzi na jinsi zinavyohusishwa katika ujifunzaji. Lazima mwalimu aelewe msukumo wa mazingira na jinsi ujifunzaji hutokea kwa hatua kutegemea umri wa mwanfunzi. Skinner (2003), anaendelea kusema kuwa, mwalimu bora lazima atilie maanani matumizi ya vifaa ambavyo vinaweza kumsaidia mwanafunzi kuelewa na kuweka kumbukumbu ya yale aliyojifunza. Skinner (2003), anamtambua mwalimu kama mwelekezi anayemsaidia mwanafunzi kutagusana na mazingira kwa minajili ya kujifunza

kupitia matumizi mwafaka ya vifaa. Utafiti huu ulilenga kupima iwapo mapendekezo haya ya Skinner (2003), yanazingatiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ni: tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo.

Kwa mujibu wa Grove (2008), picha ni muhimu na lazima zitumike katika ufundishaji wa vipengele vya lugha. Anasema kuwa, ikiwa mwalimu ataweza kutumia picha kwa hali ya uchangamfu na ucheshi wanafunzi watalichangamkia somo la sarufi. Akithibitisha umuhimu wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, (Grove 2008) anakiri kuwa, kanda za video ni muhimu katika ufundishaji kwa kuwa hunasa na kueleza picha inavyonuiwa kuelezwa. Mwalimu huweza kubadili njia na mtindo wa kufunza na kubadili mazingira ya darasani kwa upesi kama ilivyotarajiwa. Kanda za video huibua hisia za mwanafunzi, humzuzua kimawazo, hupunguza uchovu na kumpa motisha kuendelea kujifunza.

Mapendekezo haya ya Grove (2008), yanachangia utafiti huu kwa kuwa, matumizi ya picha na kanda za video katika ufundishaji na ujifunzaji hudhihirisha usasa katika shughuli hii. Hata hivyo, tofauti ni kuwa utafiti huu ulilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Wakidhihirisha umuhimu wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji, Marine na Hilles (2008), wanaeleza kuwa, vifaa vya kusikiliza na kutazama ni vyombo vinavyotazamwa kwa macho na kutoa sauti ili kuwasilisha ujumbe. Vifaa hivi ni muhimu katika somo la sarufi ya Kiingereza kwa kuwa husaidia kuhifadhi hali ya juu ya motisha katika somo. Wanaendelea kusema kuwa, vifaa hivi vina uwezo wa kukuza usomaji wa lugha na

kuufanya uwe wa kusisimua. Maoni ya wataalamu hawa, yanachangia utafiti huu kwa kuwa wanaeleza kuhusu matumizi ya vifaa vya kusikiliza na kutazamwa. Tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo ni vifaa vya kutazamwa na kusikilizwa. Hata hivyo, tofauti ni kuwa, wasomi hawa wanatoa maoni kuhusu matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kingereza ilhali utafiti wangu ulilenga kutathmini vifaaa vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili.

Isitoshe, Nunan (2004), anatambua kuwa, asilimia kubwa ya ujumbe tunaowasilisha hupitishwa kwa kutumia hisi ya kuona na inayosalia ni kupitia hisi ya kusikiliza. Anaendelea kufafanua kuwa, kutumia hisi ya kuona katika mawasiliano ni jambo muhimu sana. Hii ni kwa sababu, watu huhifadhi asilimia ishirini ya wanachokisikia na asilimia hamsini ya mawasiliano yanapohusisha hisi ya kuona na kusikia. Vifaa vya kufundishia ni muhimu na vinasaidia katika kufasiri ujumbe. Mapendekezo haya ya Nunan (2004), yanachangia utafiti huu kwa kuwa ulilenga kupima umuhimu wa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Naye Ngonga (2002), akichunguza mbinu bora za kufundishia somo la Kiingereza katika Wilaya ya Maseno, anathibitisha kuwa, mbinu bora ya ufundishaji wa Kiingereza ni ile inayohusisha matumizi ya vifaa katika shughuli nzima ya ufundishaji. Anasisitiza kuwa, vifaa vinavyohusisha teknolojia ya kisasa hurahisisha uelewekaji wa dhana. Utafiti wangu ulilenga kupima iwapo matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo huweza kuleta matokeo bora katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben kama anavyohoji Ngonga (2002).

## 2.5 Tafiti Kuhusu Matumizi Bora ya Vifaa vya Ufundishaji

Oginga (2010), anasema kuwa, matumizi ya vifaa yanafaa yaambatane na matayarisho bora. Mwalimu anafaa kujifahamisha na mahitaji ya silabasi kuhusu matumizi ya vifaa katika ufundishaji. Matumizi ya vifaa inavyostahili ni jambo ambalo linastahili kutiliwa maanani ili kufanikisha somo. Iwapo matumizi ya vifaa hayatafanywa kwa njia bora, vifaa hivyo havitasaidia kuafikia malengo ya mwalimu na mwanafunzi. Utafiti wangu ulilenga kutathmini iwapo walimu wanazingatia mapendekezo haya ya Oginga (2010), katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo.

Naye Robinson (1980), anasema kuwa, uteuzi wa vifaa hutegemea shabaha za mada husika, malengo ya mwalimu, jinsi zitakavyowasaidia kutagusana na umri wa wanafunzi. Ornestein (1990), vile vile, ana maoni kuwa uteuzi wa vifaa pia hutegemea ujuzi na tajriba ya mwalimu, kuwepo kwa malighafi ya kutumia, malengo ya somo na kiwango cha wanafunzi. Malengo ya somo yanafaa yawe wazi na rahisi kueleweka. Mwalimu anafaa kutilia maanani kuwa kifaa kimoja kinaweza kutumiwa kuafikia malengo kadhaa. Kwa kutilia maanani maoni haya ya Robinson (1980), utafiti huu, ulilenga kutathmini jinsi walimu huandaa vipindi vya sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ni tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo.

Kwa mujibu wa Oginga (2010), muundo au umbo la kifaa ni suala muhimu la kuzingatiwa wakati wa uteuzi wake. Vifaa bora huwa vya kuvutia, vyenye ukubwa wa kuridhisha na vyenye vielelezo na mapambo ya kuvutia. Mapambo yawe na dhima ya mafunzo wala yasiwe kikwazo cha uzingativu na usikilizaji. Anaendelea kusema kuwa, wanafunzi wanafaa kuandaliwa vilivyo kuhusu kile ambacho wanaenda kuona ama

kusikiliza. Maelezo mafupi yanafaa kutangulia matumizi ya vifaa vya ufundishaji. Utafiti huu ulilenga kupima iwapo maelekezo haya ya Oginga (2010), yanazingatiwa na walimu katika kaunti ndogo ya Moiben wanapofundisha sarufi kwa kutumia tarakilishi, na vipakatalishi vinapounganishwa na vinuruweo.

Wakati huo huo, Kawoya (2012), anasema kuwa, malengo ya somo huathiri matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Anahoji kwamba, kabla ya kukagua kifaa cha kutumia katika ufundishaji, mwalimu anafaa kutathmini malengo yake ya somo. Kwa kufanya hivi, mwalimu atahakikisha kuwa kifaa hiki kinamsaidia mwalimu kuwasilisha somo lake na kulifanya kueleweka kwa urahisi. Utafiti huu ulilenga kubaini iwapo walimu katika kaunti ndogo ya Moiben wanazingatia matayarisho haya wanapotumia tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo kufundisha sarufi.

Naye Dale (1969), akiorodhesha mambo ya kuzingatiwa wakati wa kuandaa vifaa vya kufindishia, anahoji kuwa lazima mwalimu azingatie ukubwa wa zana, idadi ya wanafunzi na maudhui ya somo. Aidha, anatoa ushauri kwa walimu kwamba, kabla ya kuteua wazingatie mahitaji ya mada husika kwa kuwa kila mada huwa na mahitaji yake. Vile vile, walimu wazingatie shabaha ya somo. Vifaa vichaguliwe kulingana na shabaha ya somo husika. Isitoshe, mwalimu anafaa kuzingatia muda uliopo, ufaafu wa vifaa kwa kupitisha maudhui ya somo, gharama ya vifaa na uwezo wa wanafunzi.

Dale (1969), anazidi kuhoji kwamba walimu wanafaa kuzingatia mahusiano ya vifaa darasani, kuwepo kwa kawi au nguvu za umeme na mwelekeo wa mwalimu na mwanafunzi kuhusiana na matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kuzingatia ushauri huu wa Dale (1969), utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi walimu

katika kaunti ndogo ya Moiben wanatumia vifaa vya kisasa ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi, vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Isitoshe, Aggarwal (1995), anajadili kuhusu sifa za vifaa vizuri vya kufunzia. anasema kuwa, kifaa kizuri kinafaa kiwe na uhusiano na mada inayofundishwa. Kifaa kizuri hulingana na somo, hueleweka kwa urahisi na maandishi yake husomeka kwa urahisi. Anamshauri mwalimu kuvitumia vifaa vitakavyomsaidia kufaulisha somo lake kwa urahisi na kuwasaidia wanafunzi kulielewa somo lake kwa haraka. Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben wanazingatia maelekezo ya Aggrawal (1995) wanapofundisha sarufi kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo.

Ili kuhakikisha matumizi bora ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, Koross na Murunga (2017), wanatoa hatua muhimu katika matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Wanasema kuwa, hatua ya kwanza ni kuwa, mwalimu wa Kiswahili aanze kwa kupitia malengo ya somo lake, kiwango cha wanafunzi lengwa, mikakati mbalimbali ya kufundisha. Kifaa cha ufundishaji kinaweza kuchaguliwa baada ya kutathmini mambo haya. Hatua ya pili ni kuamua kifaa bora cha kutumiwa katika uwasilishaji wa maudhui ya somo. Hatimaye, hatua ya tatu ni kutafuta kifaa cha kufundishia. Utafiti wangu ulilenga kuchunguza iwapo walimu wanaofundisha Kiswahili katika kaunti ya Moiben wanazingatia hatua hizi wanapofundisha sarufi kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo.

## 2.6 Tafiti Kuhusu Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Kwa mujibu wa Koross na Murunga (2017), teknolojia ni kigezo muhimu katika elimu na hasa ufundishaji wa somo la Kiswahili. Wanahoji kuwa kuenea kwa tarakilishi pia kunamaanisha kuongezeka kwa programu za kompyuta na kuongeza habari mtandaoni. Wanaendelea kusema kuwa, matumizi ya teknolojia kama vile virusha maandishi (powerpoint) na ubao mweupe yanafaa kuzingatiwa katika vipindi vya Kiswahili ili kunasa akili za wanafunzi darasani. Maoni haya ya Koross na Murunga (2017), yaliongoza utafiti huu katika kuchunguza jinsi vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Abuyeka (2014), alitafitia matumizi ya vifaa vya kompyuta katika ufundishaji wa Kiswahili. Utafiti wake ulilenga kuchunguza matumizi ya visaidizi vya kompyuta kufundisha somo la Kiswahili kwa jumla katika shule za sekondari. Kwa mujibu wa Abuyeka (2014) visaidizi vya tarakilishi vilivyotumika mara kwa mara ni sidii na dividii. Walimu walitumia vifaa hivi kuhifadhi nukuu na kuandaa maazimio ya kazi. Walimu hawakuvitumia visaidizi vya tarakilishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Alibaini kuwa walimu hawakuwa na motisha wa kuhusisha visaidizi vya tarakilishi katika ufundishaji wao.

Akithibitisha changamoto hii Abuyeka (2014), anasema kuwa, asilimia 8% ya walimu walivitumia vifaa hivi. Matokeo yaliendelea kudhihirisha kuwa visaidizi hivi vilitumika kufundisha kipengele cha kusikiliza na kuzungumza. Utafiti huu wa Abuyeka (2014), ulilenga vifaa vya kisasa. Hata hivyo, ulilenga matumizi ya visaidizi vya tarakilishi pekee. Isitoshe ulilenga ufundishaji wa Kiswahili kwa jumla kinyume na utafiti wangu

ambao ulilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Naye Githinji (2016), alichunguza mambo yanayoathiri uhusishaji wa vifaa vya kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji wa sayansi katika kaunti ya Muranga. Kwa mujibu wa Githinji (2016), asilimia 36% ya walimu hawatumii vifaa vya kidijitali katika ufundishaji wao. Asilimia 68% walikiri kuwa hawana vifaa vya kidijitali katika shule zao. Githinji (2016), aliendelea kuthibitisha kuwa vifaa vya kidijitali vilitumika mara nyingi katika kidato cha tatu na cha nne. Ilibainika vile vile kuwa, walimu hawana weledi katika uhusishaji wa matumizi ya vifaa vya kidijitali katika ufundishaji wa sayansi. Kinyume na utafiti huu uliolenga sarufi ya Kiswahili, utafiti wa Githinji (2016), ulilenga somo la Sayansi katika shule za upili zilizoko kaunti ya Muranga.

Vile vile, Kareji (2016), alihakiki uhusishaji wa vifaa vya kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiingereza. Utafiti huu ulilenga kuchunguza vifaa vya kidijitali vinavyopatikana shuleni na kuhakiki vipengele vya kiingereza vinavyofundishwa kwa kutumia vifaa hivi. Utafiti huu ulibaini kuwa uhusishaji wa vifaa vya kidijitali katika kaunti Nyakach haujatiliwa mkazo. Shule nyingi hazikuhusisha vifaa hivi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kiingereza. Kwa mujibu wa Kareji (2016), mashirika yasiyo ya kiserikali yamewapa shule nyingi katika kaunti ya Nyakach vifaa hivi vya kidijitali. Hata hivyo, alithibitisha kuwa vifaa hivi havitumiki katika ufundishaji na ujifunzaji. Ilidhihirika kuwa, washikadau wa elimu katika kaunti ndogo ya Nyakach wanaunga mkono uhusishaji wa vifaa vya kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti huu wa Kareji (2016), ni tofauti na wangu, kwa kuwa alilenga ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiingereza ilhali utafiti wangu ulilenga sarufi ya Kiswahili.

Isitoshe, katika kuchunguza ufanisi wa matumizi ya vifaa vya kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la dini, Kipkoech (2017), anadai kuwa, asilimia 80% ya walimu katika kaunti ya Bomet wamepokea mafunzo kuhusiana na matumizi ya vifaa vya kidijitali. Anaendelea kusema kuwa, asilimia 4% ya walimu katika kaunti hiyo ya Bomet hawajapokea mafunzo yoyote kuhusiana na matumizi ya vifaa hivi. Japo walimu wengi wamepokea mafunzo, matumizi yao ya vifaa hivi ni finyu mno. Utafiti wangu ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji katika kufundisha sarufi ya Kiswahili kinyume na utafiti wa Kipkoech (2017) ambao ulitafitia somo la dini.

Kwa mujibu wa Kimani (2015), walimu wengi hutumia mbinu ya mhadhara katika kufundisha sarufi huku mbinu za kisasa zinazowashirikisha wanafunzi zikipuuzwa. Ubao na chaki pekee hutumika katika ufundishaji. Kwa hivyo, wanafunzi hawafurahii masomo ya sarufi na hatimaye matokeo hayaridhishi. Kimani (2015), alilinganisha mbinu za kufundishia sarufi na umilisi wa mazungumzo kwa wanafunzi. Alichunguza matumizi ya vifaa kongwe kama mojawapo ya mbinu za kufundishia sarufi. Vifaa alivyovichunguza katika utafiti wake ni matumizi ya ubao, chaki, vitabu vya kiada na chati. Utafiti wake ulithibitisha kuwa vifaa hivi kongwe vinatumika katika kufundisha sarufi. Hata hivyo, anapendekeza kuwa ili kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi, mwalimu hana budi kutumia vifaa vya kisasa. Utafiti wa Kimani (2015), ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa utafiti wangu ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na kinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben.

Naye Wambui (2015), akishadidia matokeo ya Kimani (2015), anasema kuwa, ubao na chaki vilitumika sana katika kufundisha msamiati katika shule za msingi. Kwa hivyo,

wanafunzi hawakupata msingi bora wa lugha katika shule za msingi. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya vifaa ambavyo ni: matumizi ya vinyago, video na chati kinyume na utafiti wangu ambao ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo ni: matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika kufundisha na kujifunza sarufi. Wambui (2015), alipendekeza kuwa, walimu wanafaa kutumia vifaa na kuingiza usasa katika matumizi haya ya vifaa. Utafiti huu ulitathmini usasa huu kwa kuchunguza matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Kulingana na Akung'u (2014), walimu hutumia vifaa vya aina mbili pekee. Vifaa hivi ni chati na chaki. Vifaa hivi viwili hutumika ziadi katika ufundishaji na ujifunzaji. Walimu hawatumii vifaa vingine vinavyoweza kukuza ubunifu. Utafiti wa Akung'u (2014), unahusiana na utafiti wangu kwa kuwa ulichunguza jinsi vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji huathiri matokeo ya mitihani ya kitaifa. Hata hivyo, utafiti wa Akung'u (2014), uliegemea matumizi ya vifaa kongwe haswa matumizi ya chati, kadi za maneno na vitabu vya kiada. Utafiti huu ulilenga matumizi ya vifaa vya kisasa. Ulilenga haswa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Makokha (2015), alichunguza matumizi ya vifaa katika ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili katika shule za Sekondari katika kaunti ya Nandi kaskazini. Utafiti huu wa ulilenga matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Makokha (2015), alithibitisha kuwa, matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji huwa na umuhimu mkubwa katika kuinua viwango vya uelewa wa masomo ya ushairi. Hata hivyo, anathibitisha kuwa, vifaa vilivyotumika mara nyingi ni vifaa kongwe ambavyo havikuhusisha teknolojia ya kisasa.

Aligundua kuwa, vifaa vilivyotumika mara nyingi ni chati, majarida, vitabu vya kiada na magazeti. Matokeo haya yanathibitisha kuwa pana haja ya kuingiza usasa katika shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya vifaa vya kisasa haswa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika kaunti ndogo ya Moiben kinyume na utafiti wa Makokha (2015), ambao ulilenga matumizi ya vifaa katika kufundisha kipengele cha ushairi.

Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2013), kinuruweo ni kifaa ambacho kinaweza kutumiwa na mwalimu kufundisha. Kwa kutumia mbinu hii kipakatalishi hutumiwa pamoja na kinuruweo kurusha mwanga kwenye utando. Mwanga huo unaweza kurusha maneno, majedwali au picha. Mwalimu huandaa nukuu, michoro, majedwali pamoja na picha kwa kutumia kipakatalishi. Kinuruweo humsaidia mwalimu kurusha yote aliyoyaandaa kwa ajili ya wanafunzi kuandika au kusoma ili waweze kushiriki katika somo husika. Utafiti huu ulilenga kuthibitisha matumizi haya katika shule za sekondari zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben.

## 2.7 Tafiti Kuhusu Changamoto za Matumizi ya Vifaa katika Ufundishaji

Kwa mujibu wa Mogeni (2005), ukosefu wa vitabu vya kiada ni mojawapo ya changamoto za matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Mogeni (2005), anahimiza matumizi ya vitabu vya kiada kwa kuwa hufidia maelezo ya mwalimu darasani. Mogeni (2005), alitafitia matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji ambavyo ni vitabu vya kiada. Alibaini kuwa kuna ukosefu wa vitabu vya kiada katika shule nyingi za upili nchini Kenya. Utafiti wa Mogeni (2005) ulilenga matumizi vitabu vya kiada pekee ilhali utafiti huu ulilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi na

vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji. Vile vile, utafiti wa Mogeni (2005), ulilenga vitabu vya kiada vinavyotumika katika masomo yote kinyume na utafiti wangu ambao ulilenga kipengele cha lugha ambacho ni sarufi. Utafiti huu ulichunguza changamoto zinazokumba matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben.

Nao Njogu na Nganje (2012), katika utafiti wao, wanalalamikia jinsi walimu huchagua vifaa vya kufunzia Kiswahili na pingamizi za utumiaji wa vifaa hivyo. Wanahoji kuwa, kuna ukosefu wa kuwa makini katika utengenezaji wa vifaa vya kufundishia, mielekeo hasi ya walimu katika kutengeneza vifaa vya kufundishia Kiswahili na ukosefu wa sehemu za kuhifadhi vifaa vichache vilivyotengenezwa au kununuliwa. Utafiti huu ulilenga kutathmini changamoto zinazokumba matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Tofauti kati ya utafiti wangu na ule wa Njogu na Nganje (2012), ni, upeo na mipaka ya utafiti. Wataalamu hawa walitafitia kifaa mahususi ambacho ni redio. Utafiti wangu ulitathmini matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben.

Isitoshe, Onyango (2009), anakiri kuwa, kuna uhaba wa nyenzo za aina mbalimbali za kufundishia katika shule za msingi katika manispaa ya Kakamega. Nyenzo zilizokuwepo hazikutumika katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kutilia maanani matokeo ya Onyango (2009), utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo uhaba wa vifaa vya kisasa unaathiri matumizi ya tarakilishi vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben.

Utafiti wa Onyango (2009), ulijikita katika matumizi ya nyenzo kwa ujumla ilhali utafiti huu ulikuwa mahususi katika kutafitia matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa kipengele mahususi cha sarufi. Isitoshe, Onyango (2009), alifanya utafiti wake katika shule za msingi ilhali utafiti wangu ulijikita katika shule za sekondari.

Nelima (2012), aliainisha mbinu zinazotumika katika kufundisha diwani teule za hadithi fupi. Aligundua kuwa, walimu hutumia mbinu ya mhadhara pekee katika kufundisha. Matokeo ya utafiti wa Nelima (2012), yalithibitisha kuwa hali hii ilisababishwa na ukosefu wa fedha za kuvinunua vifaa vya kufundishia. Alidhihirisha kuwa mbinu hii ya mhadhara iliwanyima wanafunzi fursa ya kushiriki kikamilifu katika somo. Utafiti huu wa Nelima (2012), ulilenga mbinu za ufundishaji. Matumizi ya vifaa ni mbinu mojawapo ya Ufundishaji na ujifunzaji. Tofauti kati ya utafiti huu na wa Nelima (2012) ni kuwa, utafiti wa Nelima (2012), ulilenga mbinu za ufundishaji kwa jumla ilhali utafiti wangu ulilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo pekee. Vile vile, Utafiti wa Nelima (2012), ulilenga kipengele cha hadithi fupi kinyume na utafiti huu uliolenga kipengele cha sarufi. Utafiti huu ulilenga kutathmini iwapo miaka saba baada ya utafiti wa Nelima (2012), kuna mabadiliko kuhusu changamoto za matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji.

Naye Kariuki (2017), akilalamikia changamoto za matumizi ya vifaa anasema kwamba, shule nyingi zina upungufu wa nyenzo na walimu wengi hawazitumii. Alithibitisha kuwa, walimu walikumbwa na upungufu wa muda wa kutayarisha nyenzo za kufundishia. Kariuki (2017), alifanya utafiti wake katika shule za msingi ilhali utafiti huu ulilenga

shule za upili zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben. Vile vile, Kariuki (2017), alilenga matumizi ya nyenzo za aina zote za ufundishaji na ujifunzaji ilhali utafiti huu ulitafitia vifaa vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo. Isitoshe, alitafitia matumizi ya nyenzo katika kufundisha Kiswahili kwa jumla katika shule za msingi ilhali utafiti wangu ulilenga kipengele cha Kiswahili ambacho ni sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Kwa upande mwingine, Luvisia (2003), alitafitia upatikanaji na matumizi ya nyenzo katika kufundisha sarufi ya Kiswahili katika shule za upili zilizoko katika kaunti ya Bungoma. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, nyenzo hazitumiki katika kufundisha sarufi. Nyenzo hizi vile vile hazipatikani shuleni. Licha ya changamoto hizi, u Luvisia (2003), alithibitisha kuwa, walimu wana mtazamo chanya kuhusu matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti huu ni tofauti na wa Luvisia (2003), kwa kuwa ulilenga vifaa vya kisasa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika pamoja na vinuruweo katika kufundisha na kujifunza sarufi kinyume na wa Luvisia (2003) uliolenga matumizi ya nyenzo kwa jumla katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Naye Kamotho (2001), anakubali kuwa, idadi kubwa ya wanafunzi ina athari hasi katika matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa vipindi vya Kiswahili vilifundishwa nyakati za alasiri wakati wanafunzi wamechoka. Hali hii ilichangia matokeo duni ya ufundishaji na ujifunzaji. Isitoshe, walimu hawakuhusisha vifaa vinavyoteka makini ya wanafunzi kufundisha. Matumizi ya vifaa vya kisasa huweza kuleta uchangamfu darasani na kuwafanya wanafunzi kushiriki ipasavyo katika somo na hivyo kuuondoa uchovu. Utafiti huu ulilenga kutathmini

umuhimu matumizi ya tarakilishi, kipakatalishi na kinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

Kulingana na Abuli (2013), vifaa vya kisasa havitumiki katika ufundishaji. Vifaa vinavyotumika ni kongwe mno. Abuli (2013), anasema kuwa, ukosefu wa matumizi ya vifaa vya kutazamwa ni masikitiko makubwa sana kwa walimu ambao wanasisitiziwa kuhusu matumizi yake ili kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti huu wa Abuli (2013),ulilenga vifaa vyote vya kutazamwa katika shule za msingi kinyume na utafiti huu ambao ulilenga vifaa vitatu vya kutazamwa ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na kinuruweo. Isitoshe, utafiti wangu ulilenga ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi pekee kinyume na wa Abuli (2013), uliolenga masomo yote ya shule za msingi.

Kutokana na uhakiki huu wa maandishi, ni wazi kwamba kuna pengo linalohitaji kujizibwa katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi. Matokeo ya tafiti za wataalamu katika uhakiki huu umethibitisha kuwa wanafunzi hawafanyi vizuri katika somo la sarufi. Aidha watafiti wengi wametafitia matumizi ya vifaa vya kimapokezi wala si vifaa vinavyohusisha teknolojia ya kisasa. Kwa hivyo ili kuziba pengo la matokeo yasiyoridhisha katika masomo ya sarufi, mtafiti alichunguza matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji yanaweza kuinua viwango vya ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imehakiki yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Katika uhakiki huo, imeangazia mbinu za ufundishaji wa sarufi, aina za vifaa vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji na umuhimu wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, imezungumzia matumizi bora ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji na changamoto zinazokumba matumizi ya vifaa hivi vya ufundishaji. Sura inayofuata imeangazia mbinu zilizotumika katika utafiti huu. Sura hiyo vile vile, imezungumzia eneo la utafiti, usampulishaji, njia za kukusanya data na vifaa vya kukusanyia data hizo. Wakati huo huo, imeangazia utafiti mwigo, unukuzi wa data na uwasalishaji na uchanganuzi wa data. Hatimaye, imejadili maadili ya utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia imejadili tahakiki ya maandishi kuhusu mada ya utafiti. Sura hii ya tatu, imeshughulikia muundo wa utafiti. Hapa, mtafiti amefafanua sababu za kuchagua eneo la utafiti. Pia mbinu za usampulishaji zimeshughulikiwa. Isitoshe, sura hii imeshughulikia mbinu za ukusanyaji, uwasilishaji na uchanganuzi wa data, maadili ya utafiti na utafiti mwigo.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Mtafiti alitumia muundo wa kimfano. Kwa mujibu wa Borg na Gall (1989), muundo wa kimfano huchunguza matukio ya hali halisi nyanjani. Muundo huu hutoa uchanganuzi wa kundi linalotafitiwa namna wanavyotekeleza shughuli inayotafitiwa. Kwa muundo huu huwasilisha data inayoaminika zaidi. Borg na Gall (1989), wanaendelea kusema kuwa muundo huu hutegemea ithibati ya hali ilivyo nyanjani. Aidha, kupitia utafiti wa kimfano, maoni na mapendekezo ya kuboresha taaluma yoyote hupatikana.

Mtafiti alizingatia muundo huu ili kupata data ya hali halisi kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Vile vile, alihusisha muundo huu ili kutoa maoni na mapendekezo ya kuboresha taaluma ya ufunzaji na ujifunzaji

## 3.3 Eneo la Utafiti

Mtafiti alifanya utafiti katika kaunti ndogo ya Moiben iliyoko katika kaunti ya Uasin Gishu (Rejelea kiambatisho I). Kaunti ya Uasin Gishu ina kaunti ndogo tano, nazo ni : Moiben, Turbo, Ainabkoi, Kesses na Soy. Eneo la Moiben lilichaguliwa kimakusudi

kuwakilisha maeneo mengine nchini Kenya yenye sifa sawa za ufundishaji na ujifunzaji. Moiben ni moja kati ya kaunti ndogo za Kaunti ya Uasin Gishu nchini Kenya ambapo ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi unaegemea mitalaa ya kitaifa ambapo ilitarajiwa kuwa kuna matumizi ya vifaa vya kisasa. Moiben ina shule za upili ishirini na sita. Kaunti ndogo ya Moiben ilichaguliwa kwa kuwa mtafiti hajakutana na utafiti wa hivi karibuni uliohusiana na matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi.

Vile vile, eneo hili linajumuisha watu wa jamii ya Kalenjin. Jamii ya Kalenjin ni mojawapo kati ya kundi la Nilotiki. Kiswahili ni lugha ya Kibantu kwa hivyo watu wa kundi la nilotiki hupata changamoto tele katika Lugha ya Kiswahili. Eneo hili lilichaguliwa kwa kuzingatia kigezo hiki.

Eneo hili linajumuisha shule moja ya kitaifa, shule za viwango vya zaidi ya kaunti tano, shule za viwango vya kaunti kumi na mbili na za kaunti ndogo nane. Aidha walimu wanaofundisha katika shule hizi ni walimu waliohitimu katika taaluma ya ufundishaji. Kutokana na uchunguzi awali wa upimaji wa vifaa vya utafiti, katika kaunti ndogo ya Moiben, ilibainika kwamba eneo hili lilikuwa na aina ya data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti.

### 3.4 Usampulishaji

Kothari (2004), anasema kuwa, usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa. Naye Sharman (1983), anasema kuwa, uteuzi wa sampuli ni sehemu ndogo ya vitu au watu wanaotafitiwa ili kudhihirisha sifa sawa za idadi kubwa ya vitu au watu inayowakilisha ili kupata matokeo yanayoweza kuaminika. Utafiti huu ulilenga shule kumi na tano kati ya shule ishirini na sita zilizoko katika kaunti ndogo ya Moiben.

Mtafiti alihusisha shule ya kitaifa, za viwango vya zaidi ya kaunti, za viwango vya kaunti na za viwango vya kaunti ndogo ili kupata data toshelevu. Utafiti ulihusisha shule moja ya kitaifa ambayo ni shule ya wasichana ya Moi. Shule tatu za viwango vya zaidi ya kaunti kati ya tano, shule saba za viwango vya kaunti kati ya kumi na mbili na shule nne za viwango vya kaunti ndogo kati ya nane. Shule hizi zilichaguliwa ili kuwakilisha shule zingine katika Kaunti ya Uasin Gishu zenye sifa sawa.

Mtafiti alitumia usampulishaji wa kimakusudi na kinasibu. Mugenda na Mugenda (1999), wanaeleza mbinu ya uteuzi wa sampuli kimakusudi kama mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuchukua data kutoka kwa watafitiwa kulingana na madhumuni ya utafiti wake. Shule ya wasichana ya Moi iliteuliwa kimakusudi kwa kuwa ni shule ya kitaifa pekee katika kaunti ndogo ya Moiben. Kwa hivyo, ilitarajiwa kuwa kuna matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji. Shule za viwango vya zaidi ya kaunti, za viwango vya kaunti na za viwango vya kaunti ndogo ziliteuliwa kinasibu.

Ili kupata ni shule gani za viwango vya zaidi ya kaunti zilihusishwa katika utafiti bila mapendeleo, kwanza mtafiti aliandika majina yote ya shule za zaidi ya kaunti kwenye vijikaratasi vidogo. Kisha vijikaratasi hivi viliwekwa kwenye debe moja. Asilimia 30% ya shule iliteuliwa kinasibu kutoka sampuli hii kama wasemavyo Mugenda na Mugenda (1999). Kutokana na uteuzi huu wa kinasibu, shule tatu za viwango vya zaidi ya kaunti ziliteuliwa na kuhusishwa katika ukusanyaji wa data. Hatua hii ilirudiwa katika kuteua asilimia 30% za shule za kaunti na za kaunti ndogo. Hivyo, shule saba za kaunti na nne za kaunti ndogo zilihusishwa katika ukusanyaji wa data.

Walimu wa Kiswahili waliohusishwa katika utafiti waliteuliwa kimakusudi. Walimu hawa waliteuliwa kimakusudi kwa kuwa wao hufundisha sarufi. Kwa hivyo, ilichukuliwa kwamba ni weledi wa ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo. Mwalimu mmoja anayefundisha Kiswahili kidato cha tatu aliteuliwa kinasibu kama kiwakilishi katika shule zote kumi na tano zilizohusishwa katika utafiti. Wanafunzi waliolengwa katika utafiti huu walikuwa wanafunzi wa kidato cha tatu. Hii ni kwa sababu utafiti ulilenga mada za sarufi zinazofundishwa katika kidato cha tatu. Uteuzi wa sampuli kinasibu ulitumika kuwateua wanafunzi waliohusishwa katika ukusanyaji data. Wanafunzi waliteuliwa kinasibu ili kuwapa nafasi sawa ya kuhusishwa bila mapendeleo. Asilimia 30% ya wanafunzi wa kidato cha tatu waliopatikana shuleni walihusishwa katika ukusanyaji wa data.

### 3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Ukusanyaji wa data unarejelea kukusanya habari mahususi zinazolenga ama kuthibitisha au kupinga ukweli fulani Kombo na Tromp (2006). Mbinu zinazotumika kukusanya data huathiriwa na vifaa vya ukusanyaji wa data Kombo na Tromp (2006). Naye, Kothari (2004), anaeleza kuwa, mbinu za ukusanyaji data ni zana au njia anazozitumia mtafiti katika ukusanyaji data. Utafiti huu ulitumia ujazaji hojaji, uchunzaji darasani na mahojiano. Data ilihusu matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben. Data iliyokusanywa ilisaidia kujibu malengo na maswali ya utafiti.

#### 3.5.1 Uchunzaji Darasani

Kwa mujibu wa Onen (2005), uchunzaji ni ushuhudiaji wa tukio linapotendeka na kukusanya taarifa zake. Anaendelea kusema kuwa uchunzaji ni kitendo cha kuchunguza

watafitiwa wanafanya nini badala ya kuwauliza maswali. Naye Gweyi (1995), anasema kuwa, uchunzaji ni njia mwafaka zaidi kutumiwa kuchunguza uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Anaendelea kusema kuwa, uchunzaji ni muhimu sana katika utafiti kwani ndiyo ya njia pekee isiyo na ubaguzi katika kupima utendaji kazi wa mwalimu na tabia ya mwanafunzi darasani. Ni kwa msingi huu uchunzaji uliteuliwa kama mbinu mojawapo ya ukusanyaji data katika utafiti huu. Uchunzaji ulifanywa kwa walimu waliofundisha sarufi walioteuliwa ili kuthibitisha mbinu walizozitumia kufundisha sarufi. Uchunzaji huu ulifanyika mara moja. Vile vile uchunzaji ulitumika kakagua vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana shuleni.

### 3.5.2 Ujazaji wa Hojaji

Casley na Lury (1981), wanafafanua hojaji kama msururu wa maswali yaliyotungwa kuhusu kila hoja maalum ambayo humwezesha mtafiti kupata maoni au majibu kutoka kwa mtafitiwa. Hojaji ilitumika katika utafiti huu kwani ilimpa mtafitiwa uhuru wa kutoa maoni na mapendekezo yake. Hojaji hizi ziliwasilishwa moja kwa moja kwa watafitiwa ili kuhakikisha kuwa hojaji zimewafikia walengwa.

Ujazaji hojaji ulifanywa na walimu na wanafunzi wa shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Kifaa hiki kilifaa kwa vile kilipunguza muda wa kukusanya data iliyohitajika Ary na wenzake (1972). Hojaji hizi zilikuwa zimeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Mtafiti aliwapa walimu na wanafunzi hojaji baada ya kuwaelezea lengo la utafiti na kuwahakikishia kwamba habari ambazo wangetoa zingehifadhiwa kwa siri wakati na baada ya utafiti. Ingawa lengo la utafiti na hakikisho la uwekaji wa siri zilikuwa katika utangulizi wa hojaji zote, mtafiti alichukua jukumu la kuwafahamisha hayo kwa mazungumzo.

Baada ya hojaji kutolewa kwa watafitiwa, miadi iliwekwa kati ya mtafiti na watafitiwa juu ya siku ya kuzichukua hojaji hizo. Watafitiwa walipewa muda wa siku tatu ili kuzijaza hojaji hizo. Baada ya siku tatu, mtafiti alikwenda kuchukua hojaji hizo. Kabla ya kuzichukua hojaji, mtafiti alizipitia kuhakikisha kwamba zilikuwa zimejazwa kikamilifu. Mtafiti alizichukua hojaji mwenyewe. Kuzichukua mwenyewe kutoka kwa watafitiwa kulikuwa na manufaa kwa vile anavyosema Peil (1995), mtafiti mwenyewe anapochukua hojaji kutoka kwa watafitiwa, huweza kuwaomba wale ambao hawajazikamilisha inavyostahili wazikamilishe.

### 3.5.3 Mahojiano

Mahojiano ni mbinu ya kuuliza maswali ya ana kwa ana kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya data kuhusu swali la utafiti Enon (1998). Nao Mugenda na Mugenda (1999), wanasema kuwa, matumizi ya mahojiano katika utafiti ni bora kwa sababu mtafiti anaweza kujiweka katika hali halisi ya mtafitiwa na hivyo kupata data bora zaidi. Wanaendelea kusema kuwa, mahojiano yanamwezesha mtafiti kupambanua maswali ya utafiti yenye utata hivyo kumwezesha mtafitiwa kutoa majibu sahihi na yenye uwazi.

Maswali yaliyoulizwa yalimwelekeza mtafiti kuwadadisi watafitiwa kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi kuhusu matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Mahojiano yalitumika kwa walimu pekee. Walimu wanaofundisha sarufi walisailiwa kuhusu jinsi wao hutumia tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo kufundisha sarufi. Aidha, walisailiwa kuhusu umuhimu wa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji wa sarufi. Usaili huu vile vile, uliwezesha utafiti kupata data kuhusu

changamoto zinazowakumba walimu wanapofundisha sarufi kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo.

### 3.6 Vifaa vya Kukusanya Data

Creswell (2014), anasema kuwa, kabla ya kuenda nyanjani kukusanya data, ni sharti mtafiti awe na mpangilio wa vifaa vya kukusanyia data. Anasema kuwa, iwapo mtafiti atatumia uchunzaji kukusanya data, sharti awe na mwongozo wa uchunzaji. Vile vile, mpango wa kutumia mahojiano huhitaji mwongozo wa mahojiano. Aidha, ujazaji hojaji huhitaji hojaji. Kwa kuzingatia maelekezo ya Creswell (2014), mtafiti alitumia mwongozo wa uchunzaji, mwongozo wa mahojiano na hojaji kama vifaa vya kukusanya data.

#### 3.6.1 Mwongozo wa Uchunzaji

Kwa mujibu wa Gweyi (2014), mwongozo wa uchunzaji ni kifaa ambacho hutumiwa kunakili tabia na matukio ya watafitiwa nyanjani. Anaendelea kusema kuwa mtafiti hutumia maswali aliyoyaandaa awali kuthibitisha kile ambacho kinaendelea nyanjani. Mwongozo wa uchunzaji ni faafu sana katika utafiti kwa kuwa humsaidia mtafiti kurekodi habari au tabia za watafitiwa kadiri zinavyotukia Gweyi (2014).

Wakati huo huo, Kothari (2004) anatoa ushauri kwa mtafiti kuwa makini ili asirekodi matukio ya kibinafsi ya watafitiwa. Kwa hivyo, mtafiti alihakikisha kuwa anarekodi data kuhusiana na matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi pekee. Kwa kutilia maanani maelekezo ya Gweyi (2014) na Kothari (2004), mtafiti alitazama masomo ya sarufi na kutumia mwongozo ya uchunzaji kukagua vifaa vilivyotumika kufundisha na kujifunza sarufi. (Tazama

kiambatisho C na D). Alama ya kikwaju kilitumika kwenye mwongozo ya uchunzaji kuonyesha kifaa kilichotumika. Aidha mwongozo wa uchunzaji ulitumika kukagua vifaa vya kisasa vinavyopatikana shuleni. Alama ya kikwaju ilitumika kuthibitisha uwepo wa tarakilishi na vipakatalishi vinavyotumika na vinuruweo.

### 3.6.2 Hojaji

Casley na Hury (1981), wanasema kuwa, kuna aina mbili za hojaji. Nazo ni: hojaji huru na hojaji funge. Seti hizi mbili za hojaji zilitumika kama vifaa vya kukusanya data: ya walimu na ya wanafunzi. Wanafunzi wa kidato cha tatu tu ndio walipewa hojaji miongoni mwa wanafunzi. Hojaji zilizotolewa kwa walimu na wanafunzi zilikuwa na maswali funge na maswali huru. Maswali funge yalikuwa na muundo maalum ili kumpa mtafiti nafasi ya kupata majibu yasiyo na maelezo ya ndani. Maswali huru yalimpa mtafiti uwezo wa kupata data yenye undani kuhusu matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. (Rejelea kiambatisho A na B). Hojaji hizi zilipelekwa na mtafiti hadi shuleni ili kuhakikisha uaminfu.

Hojaji ya mwalimu ililenga kukusanya data kuhusu jinsi walimu hutumia tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Isitoshe, Hojaji ya mwalimu iliwezesha kupatikana kwa data kuhusu umuhimu wa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Kupitia hojaji ya mwalimu, utafiti ulipata data kuhusu changamoto zinazowakumba wanapofundisha sarufi kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo.

Hojaji ya mwanafunzi iliwezesha kupatikana kwa data kuhusu jinsi wanafunzi hutumia tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo. Aidha, ilikusanya data kuhusu umuhimu wa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Vile vile ilikusanya data kuhusu na changamoto za matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben.

### 3.6.3 Mwongozo wa Maswali ya Mahojiano

Kothari (2004), anasema kwamba, mwongozo wa mahojiano ni kifaa cha utafiti ambacho hutumiwa na mtafiti kukusanya data kutoka kwa watafitiwa kwa kutumia mazungumzo ya ana kwa ana. Mwongozo wa mahojiano hutumiwa kurekodi majibu kutoka kwa watafitiwa. Kwa mujibu wa Kothari (2004), mwongozo wa mahojiano ni faafu kwa kuwa humwezesha mtafiti kupata taarifa ambazo haziwezi kuchunzwa moja kwa moja. Vile vile, humwongoza mtafiti kupata historia ya habari inayohitajika. Mwongozo wa mahojiano humpa mtafiti nafasi ya kuthibiti mahojiano baina yake na mtafitiwa.

Mwongozo wa mahojiano ulitumika kupata ufafanuzi wa ziada kutoka kwa walimu wanaofundisha sarufi. (Rejelea kiambatisho E). Mwongozo huu ulilenga kupata habari kuhusu jinsi walimu hutumia vifaa vya kisasa kufundisha sarufi. Vile vile, ulilenga kupata taarifa kuhusu umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa. Isitoshe, ulidhamiria kupata data kuhusu changamoto za matumizi ya vifaa vya kisasa.

## 3.7 Utafiti Mwigo

Mugenda na Mugenda (1999), wanahoji kuwa, lazima vifaa vya utafiti vifanyiwe majaribio ili kuhakikisha kuwa vina uwezo wa kukusanya data inayohitajika.

Wanaendelea kusema kuwa, umuhimu wa utafiti awali ni kudhibiti vifaa vya utafiti ili kuhakikisha kuwa havina kasoro. Uteuzi wa sampuli kimakusudi ulitumika kuchagua shule ya wavulana ya Chebisaas ili kufanya majaribio ya vifaa vya utafiti. Hii ni kwa sababu shule hii huandikisha matokeo bora katika mitihani ya kitaifa. Hivyo iliaminika kuwa vifaa vya kisasa vinapatikana na vinatumika katika ufundishaji na ujifunzaji.

Shule ya Chebisaas haikuhusishwa katika utafiti kamili. Wanafunzi waliojaza hojaji ni wanafunzi wa kidato cha tatu na waliteuliwa kinasibu. Walimu waliojaza hojaji ni walimu wanaofundisha Kiswahili katika kidato cha tatu na waliteuliwa kimakusudi kwa sababu wao wanafundisha sarufi, hivyo ni weledi wa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji. Maswali ambayo yalionekana kutowezesha utafiti kupata data faafu, yaliondolewa. Hali hii iliimarisha uaminifu na uthabiti wa vifaa vya utafiti.

Utafiti mwigo ulisaidia mtafiti kupima muda wa kufanya utafiti kwa lengo la kujua iwapo muda huo ungetosha kukusanya data. Iligunduliwa kwamba, muda ulionuiwa kutumika kukusanya data (mwezi mmoja na nusu) ulikuwa mfupi. Kwa hivyo, muda huo uliongezwa baada ya utafiti mwigo. Muda huo uliongezwa kutoka mwezi mmoja na nusu hadi miezi miwili na nusu.

Aidha, utafiti mwigo ulimsaidia mtafiti kuthibitisha shule ambazo zilikuwa na vifaa vya kisasa vilivyolengwa. Vifaa hivi ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo. Shule ambazo zilikuwa na vifaa hivi zilihusishwa katika kukusanya data kuhusu jinsi walimu na wanafunzi hutumia vifaa vya kisasa vya ufundishaji kufundisha na kujifunza sarufi, umuhimu na changamoto za vifaa hivi.

### 3.8 Unukuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilihusu: upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika shule za upili, jinsi walimu na wanafunzi hutumia vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi, umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa na changamoto za matumizi ya vifaa vya kisasa katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Data iliyokusanywa ilihaririwa na kuhakikisha kuwa iliafikia malengo ya utafiti. Kabla ya kuichanganua, data hii ilipangwa na kuwekwa kwenye maandishi inavyopendekezwa na Kombo na Tromp (2006)

### 3.9 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Kombo na Tromp (2006), wanasema kuwa, uchanganuzi wa data ni uhakiki wa data iliyokusanywa kwa kutoa maelezo. Data iliyokusanywa katika utafiti huu iliwasilishwa kwa kutumia asilimia na majedwali. Hatimaye data hii ilichanganuliwa kimaelezo. Data hii ilichanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi yake Bruner (1966).

### 3.10 Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Mathooko (2007), maadili ni kaida zinazoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu. Mathooko (2007), anasema kuwa, maadili katika utafiti ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotangamana nao katika utafiti, uelekevu kwa nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Mwingiliano wa kimaadili na washiriki wa utafiti hujitokeza kwa namna zifuatazo: umuhimu wa heshima, ushiriki wa hiari, uhifadhi wa usalama wa taarifa binafsi na kujibu maswali ya washiriki Mathooko (2007).

Kwa mujibu wa Anol (2012), mtafiti anafaa kutilia maanani maadili ya utafiti kabla ya kukusanya data, wakati wa kukusanya data, wakati wa uchanganuzi wa data na wakati wa kuwasilisha matokeo. Anasema kuwa, kabla ya kuenda nyanjani kukusanya data, mtafiti anapaswa kupata idhini kutoka Chuo kikuu anachosomea. Aidha, mtafiti apate barua ya idhini kutoka uongozi wa eneo la utafiti. Wakati wa kukusanya data, mtafiti anafaa kuheshimu tamaduni za watafitiwa, kuwajulisha watafitiwa lengo lake la kukusanya data na kuhakikisha kuwa kuna usawa kwa watafitiwa wote. Anol (2012), anaendelea kuhoji kuwa wakati wa uchanganuzi wa data, usiri wa taarifa zilizotolewa na watafitiwa unafaa kutiliwa maanani. Isitoshe, anamshauri mtafiti kwamba wakati wa uwasilishaji wa matokeo, mtafiti asiwasilishe matokeo chanya pekee bali awasilishe matokeo chanya na hasi.

Kutokana na maelekezo ya Anol (2012), mtafiti alifanya utafiti baada ya kupata idhini ya kufanya utafiti kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Kisayansi na Teknolojia (National Council for Science and Technology). Kwa mujibu wa Trochim (2002), mtafiti anafaa kuandaa kikao na watafitiwa na kuwajulisha kusudi lake. Kwa kutilia maanani maelekezo haya ya kimaadili, mtafiti aliandaa kikao kisha akawaelezea watafitiwa azma yake kuu ya ukusanyaji data na kuwaomba idhini ya kuwashirikisha.

Kwa kuzingatia maelekezo ya Mathooko (2007), uhifadhi wa usalama wa taarifa binafsi ulihakikishwa kwa kuwa watafitiwa hawakuhitajika kuandika majina yao kwenye hojaji. Taarifa zilizotolewa zilitumiwa katika utafiti pekee. Mtafiti alihakikisha kuwa data aliyokusanya ni ile ambayo ilitolewa na watafitiwa ambao walikubali kushiriki katika utafiti. Mligo (2012), anasema kuwa, wizi wa kitaaluma ni kinyume cha maadili ya uandishi. Anasema kuwa, wizi wa kitaaluma huhusisha wizi wa maneno, mawazo au

vifungu vya maneno kutoka kwa watafiti au watu wengine bila kuonyesha ni ya nani na chanzo chake. Mtafiti aliepukana na wizi wa kitaaluma kwa kutambua mchango wa waandishi wengine na vyanzo vyote vya mawazo yao kwa kufanya unukuzi sahihi wa maandishi yao.

## 3.11 Matatizo katika Utafiti

Japo mtafiti alifaulu katika utafiti alivyopanga, matatizo hayakuweza kuepukika. Kwanza, ni kuchelewa kwa barua za utafiti. Barua kutoka Chuo kikuu cha Kibabii ilichelewa. Aidha, barua kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Kisayansi na Teknolojia ilichukua muda mrefu. Hali hii ilikwamisha utafiti huu kwa miezi kadhaa. Barua ya utafiti ni muhimu kwa kuwa humpa mtafiti ujasiri wa kufika eneo la utafiti kwa minajili ya utafiti. Bila barua ya utafiti, mtafiti hukosa imani kutoka baadhi ya walimu na walimu wakuu katika kaunti ndogo ya Moiben.

Mara nyingi walimu walikataa kushiriki katika ujazaji wa hojaji na kuhusishwa katika mahojiano. Wengi wao walidai kuwa na kazi nyingi na hivyo hawangepata nafasi ya kuhojiwa. Hata hivyo, wengine walikubali kujaza hojaji na kuhojiwa. Wanafunzi vile vile hawakujaza hojaji inavyostahili. Baadhi yao waliandika majibu yasiyohusiana na maswali ya hojaji. Hata hivyo, wengi walijibu inavyostahili na hivyo kusaidia utafiti kupata data toshelevu.

Tatizo jingine ni usafiri. Barabara nyingi katika kaunti ndogo ya Moiben, zilikuwa katika hali mbovu. Mara nyingi mtafiti alilazimika kuabiri pikipiki ili kufikia shule ambazo barabara zao zilikuwa katika hali duni. Nyakati za mvua pikipiki hazikuwepo. Mtafiti

mara nyingi alilazimika kutembea kwa miguu kilomita nyingi ili kufika shuleni kwa minajili ya kukusanya data.

Ukosefu wa maafisa wa elimu katika ofisi zao vile vile lilikuwa tatizo. Mara nyingi mtafiti alisafiri mjini Eldoret kwa lengo la kuomba barua ya ramani ya kaunti ndogo ya Moiben na orodha ya shule. Mara kwa mara maafisa hawakuwepo. Hata hivyo, hatimaye mtafiti aliweza kupata ramani ya Kaunti ndogo ya Moiben na orodha ya shule katika kaunti hii.

Tatizo jingine ni kuwa wakati wa utafiti, mtafiti alikuwa anahudumu kama mwalimu wa Kiswahili katika shule ya wavulana ya Arnesen's. Ilikuwa changamoto kusawazisha shughuli hizi mbili. Ruhusa za mara kwa mara aghalabu zilimkera mkuu wa idara ya Kiswahili. Wakati wa ukusanyaji wa data, mtafiti alilazimika kufundisha usiku na mapema asubuhi ili kuenda nyanjani kukusanya data mchana. Hata hivyo, mtafiti alikabili tatizo hili na kuweza kukusanya data ipasavyo.

### 3.12 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia muundo wa utafiti. Vile vile, imezungumzia kuhusu eneo la utafiti, usampulishaji, ukusanyaji data na vifaa vya kukusanya data. Aidha utafiti mwigo umeangaziwa katika sehemu hii. Unukuzi wa data iliyokusanywa, uwasilishaji na uchanganuzi wa data umeshughulikiwa katika sura hii. Hatimaye, sehemu hii imezungumzia maadili ya utafiti ambapo masuala ya kimaadili katika utafiti yamezungumziwa. Sura inayofuata inawasilisha na kuchanganua data iliyokusanywa kuhusiana na matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumiwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia imezungumzia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sehemu hii inangazia uwasilishaji, uchanganuzi wa data na kujadili kuhusu matokeo ya utafiti. Uchanganuzi huu umeongozwa na malengo ya utafiti ambayo ni: Kuthibitisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya ufundishaji katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben, kuchunguza jinsi walimu hutumia tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi, kuhakiki umuhimu wa ufundishaji wa sarufi kwa kutumia vifaa vya kisasa na kutathmini changamoto zinazokumba matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji katika kufundisha na kujifunza sarufi.

## 4.2 Upatikanaji wa Vifaa vya Ufundishaji kwa Ujumla

Mtafiti alitaka kuthibitisha vifaa vinavyotumika mara nyingi katika ufundishaji na ujifunzaji katika shule za upili za kaunti ndogo ya Moiben. Lengo lilikuwa ni kuthibitisha iwapo vifaa vya kisasa kama vile tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika pamoja na vinuruweo vinapatikana katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Matokeo yamedhihirishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.1: Vifaa vya Ufundishaji Vinavyopatikana katika Shule za Upili**

| Kifaa | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Ubao | 15 | 100% |
| Picha | 12 | 80% |
| Chati | 15 | 100% |
| Vifaa halisi | 3 | 20% |
| Filamu | 4 | 26.67% |
| Vitabu vya kiada | 15 | 100% |
| Ramani | 4 | 26.67% |
| Runinga | 4 | 26.67% |
| Tarakilishi | 8 | 53.33% |
| Vipakatalishi | 9 | 60% |
| Redio | 6 | 40% |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Kutokana na jedwali 4.1, matokeo yalithibitisha kuwa, asilimia 100 (N=15) ya walimu ilitumia ubao kama kifaa kikuu cha kufundishia. Hali hii ilitokana na ukosefu wa fedha shuleni za kuvinunua vifaa vya kisasa vya kufunzia. Nayo asilimia 80 (N=12) ya walimu waliohojiwa ilitumia picha kama kifaa cha kufundishia kufundisha. Kando na ubao kifaa kinachotumika zaidi ni chati. Asilimia 100 (N=15) ya walimu walitumia chati kama kifaa cha kufundishia. Matokeo haya yanashabihiana na matokeo ya Wambui (2015), ambaye

katika utafiti wake alibaini kuwa walimu wengi walitumia chati kama kifaa kikuu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Vifaa halisi vilitumiwa na asilimia 20 (N=3) ya walimu. Vifaa halisi ni vitu na shughuli ambazo hutumiwa darasani kuhusisha ufindishaji na ujifunzaji. Vile vile, asilimia 26.67 (N=4) ya walimu waliohojiwa ilitumia filamu katika ufundishaji wao. Filamu ilitumika kwa viwango vya chini mno ingawa inaleta uhalisia darasani anavyohoji Ornstein (1990). Aidha, asilimia 100 (N=15) ya walimu waliohojiwa ilitumia vitabu vya kiada kama vifaa vya ufundishaji. Ilibainika kuwa, vitabu vya kiada kama vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vilifaa kwa kuwa mada zote zilizo kwenye silabasi zimeelezwa kwa undani katika vitabu hivi pamoja na mbinu za kufundishia na mazoezi.

Wakati huo huo, asilimia 26.67 (N=4) ya walimu waliohojiwa ilikubali kutumia ramani katika ufundishaji wao. Matumizi ya ramani iliweza kuwasaidia wanafunzi na walimu kuona na pia kujua vile Kiswahili kilianza na kusambaa nchini. Kwa hivyo kifaa hiki hakikutumika katika kufundisha sarufi.

Vile vile, asilimia 26.67 (N=4) ya walimu waliohojiwa ilitumia runinga kama kifaa cha kufundishia. Ilibainika kwamba runinga ni kifaa muhimu sana ikitumika kufundisha kama anavyoashiria Oginga (2010) kwamba, runinga ni chombo ambacho huweza kuwafikia wanafunzi wengi kwa wakati mmoja. Walimu wanafaa kuwaandalia wanafunzi vipindi vinavyoweza kuwasaidia kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, asilimia 53.33 (N=8) ya walimu waliohojiwa ilitumia tarakilishi kama kifaa cha ufundishaji na ujifunzaji. Asilimia hii ni finyu mno kwa sababu walimu

walikosa mtandao shuleni. Kwa hivyo, walipata changamoto kutumia tarakilishi katika ufundishaji wao. Hali hii vile vile ilichangiwa na ukosefu wa fedha shuleni za kuvinunua tarakilishi. Changamoto hili linaafikiana na changamoto aliyoigundua Nelima (2012), kwamba, walimu hutumia vifaa kongwe na mbinu ya mhadhara katika ufundishaji wao kwa kuwa shule hukosa fedha za kuvinunua vifaa vya kisasa. Mbinu hii ya mhadhara huwanyima wanafunzi fursa ya kushiriki kikamilifu katika somo. Ilibainika kuwa, tarakilishi ni kifaa muhimu cha kielimu ambacho walimu wanafaa kuitumia katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kama asemavyo Papert (1987).

Nayo redio ilitumiwa na asilimia 40 (N=6) ya walimu waliohojiwa. Vipindi vya redio viliwapa wanafunzi fursa ya kufunzwa na walimu tofauti ambao pia ni wataalamu katika somo husika Odera (2007). Matokeo haya yanathibitisha kuwa vifaa vinavyopatikana na kutumika katika shule za upili za kaunti ndogo ya Moiben, vingi ni vya kimapokeo. Vifaa vinavyohusisha teknolojia ya kisasa ni vichache mno. Mwalimu katika shule ya kisasa hana budi kuhusisha vifaa vya kisasa ili kuweza kuteka ari ya mwanafunzi ya kutaka kujifunza zaidi kama inavyodhihirishwa na mhimili wa nne wa nadharia ya kujifunza kiugunduzi yake Bruner (1966).

### 4.2.2 Upatikanaji wa Vifaa vya Kisasa vya Ufundishaji na Ujifunzaji.

Mtafiti alilenga kuthibitisha upatikanaji wa tarakilishi na vipakatalishi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Matokeo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.2: Upatikanaji wa Vifaa vya Kisasa vya ufundishaji**

| Shule | Tarakilishi | Asilimia | Vipakatalishi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Moi | 2 | 25 | 3 | 33.33 |
| Kimumu | 1 | 12.5 | 0 | 0 |
| Seko | 1 | 12.5 | 1 | 11.11 |
| Eldoret ya Kati | 1 | 12.5 | 1 | 11.11 |
| Chuo Kikuu cha Eldoret | 1 | 12.5 | 1 | 11.11 |
| Itigo | 1 | 12.5 | 1 | 11.11 |
| Kuinet | 1 | 12.5 | 1 | 11.11 |
| **Jumla** | **8** | **100** | **9** | **100** |

Kutokana na jedwali 4.2, ilibainika kuwa, asilimia 46.67 (N=7) ya shule kumi na tano zilizohusishwa katika utafiti ilikuwa na vifaa vya kisasa. Shule hizi zilikuwa na vyumba vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Vyumba hivi vilikuwa na tarakilishi au kipakatalishi kilichotumika na kinuruweo. Shule hizi ni: shule ya wasichana ya Moi, shule ya upili ya Kimumu, shule ya upili ya Eldoret ya kati, shule ya upili ya Chuo Kikuu cha Eldoret, shule ya upili ya Itigo na shule ya upili ya Kuinet.

Matokeo yalithibitisha kuwa, shule ya kitaifa ya wasichana ya Moi ilikuwa na asilimia 25 (N=2) ya tarakilishi zote zilizopatikana. Uchunguzi wa vyumba vya TEHAMA vya shule ya upili ya Kimumu, Seko, Eldoret ya Kati, Chuo Kikuu cha Eldoret, Itigo na Kuinet ulithibitisha kuwa kulikuwa na asilimia 12.5 (N=1) ya tarakilishi zote zilizopatikana katika kila mojawapo ya shule hizo.

Matokeo yaliendelea kuthibitisha kuwa, katika shule ya kitaifa ya wasichana ya Moi kulikuwa na asilimia 33.33 (N=3) ya vipakatalishi vyote vilivyopatikana. Shule ya wasichana ya Seko, shule ya upili ya Eldoret ya Kati, Shule ya upili ya Chuo Kikuu cha

Eldoret, shule ya upili ya Itigo na shule ya upili ya Kuinet, zilikuwa na asilimia 11.11 (N=1) ya vipakatalishi vyote vilivyopatikana katika kila mojawapo ya shule hizo. Asilimia ya 11.11 ni finyu mno kwa walimu wanaosisitiziwa matumizi ya teknolojia katika ufundishaji wao.

Vyumba hivi vya TEHAMA, vilikuwa na vinuruweo ambavyo vilitumika pamoja na vipakatalishi kufundisha na kujifunza. Vipakatalishi pamoja na vinuruweo vilitumika kurusha maandishi kwenye ubao mweupe. Vile vile, vilitumika kurusha picha na video ambazo ziliwasaidia wanafunzi kuelewa somo kupitia uwezo wa kuona na kusikia kama inavyojitokeza katika mhimili wa tatu ya nadharia kujifunza kiugunduzi yake Bruner (1966). Matokeo haya yanaakisi maoni ya Koross na Murunga (2017), ambao wanasema kwamba, katika karne ya ishirini na moja, ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili lazima lichukue mkondo wa kuhusisha matumizi ya teknolojia ya kisasa.

### 4.3 Jinsi Vifaa vya Kisasa Vinatumika Kufundisha na Kujifunza Sarufi

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi walimu hutumia vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Vifaa hivi ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo. Idadi ya walimu waliohojiwa walikuwa saba kati ya kumi na watano.

#### 4.3.1 Jinsi Walimu hutumia Tarakilishi Kufundisha Sarufi

Mtafiti alitaka kuchunguza jinsi walimu hutumia tarakilishi kama kifaa cha kisasa kufundisha sarufi. Ili kuchunguza matumizi haya, mtafiti alilenga kuchunguza jinsi walimu hutumia tarakilishi kufundisha mada za sarufi mbazo ni: usemi halisi na usemi

wa taarifa, vielezi, uakifishaji, muundo wa sentensi, nyakati na hali. (Rejelea kiambatisho E). Matokeo yanadhihirishwa kupitia kwa jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.3: Jinsi Walimu hutumia Tarakilishi Kufundisha Sarufi**

| Mada ya sarufi. | Idadi ya walimu waliotumia tarakilishi. | Asilimia |
|---|---|---|
| Muundo wa sentensi. | 1 | 14.29% |
| Nyakati na hali | 1 | 14.29% |
| Uakifishaji | 2 | 28.57% |
| Usemi halisi na usemi wa taarifa. | 1 | 14.29% |
| Vielezi | 2 | 28.57% |
| **Jumla** | **7** | **100** |

Kutokana na jedwali 4.3, ilibainika kuwa, asilimia 14.29 (N=1) ya walimu saba waliohojiwa ilitumia tarakilishi kufundisha kipengele cha sarufi cha usemi halisi na usemi wa taarifa. Asilimia hii ilikuwa chini mno. Hali hii ilichangiwa na mtazamo hasi wa walimu wengine kuhusiana na matumizi ya vifaa vya kisasa. Kwa hivyo, Changamoto wanazozizungumzia Njogu na Nganje (2012), katika utafiti wao vile vile ziliweza kubainika. Walivyogundua kuwa walimu wana mitazamo hasi kuhusu matumizi ya redio kufundisha na kujifunza, hali hiyo ilidhihirika wazi miongoni mwa walimu wa kaunti ndogo ya Moiben. Utafiti ulibaini kuwa mwalimu huyu alitumia tarakilishi kuhifadhi semi halisi kwenye dividii na sidii ili kutumia katika ufundishaji wake. Semi za taarifa pia zilihifadhiwa kwenye vifaa hivi na kutumika darasani kufundisha usemi wa taarifa. Semi hizi zilitolewa mtandaoni. Ili kufanikisha matumizi ya tarakilishi, kinuruweo kilitumika kurusha semi hizi kwenye ubao mweupe. Matumizi haya yalibainika kuwa

muhimu katika kurahisisha ulewekaji wa usemi halisi na usemi wa taarifa. Hii ni kwa sababu, hisi ya kutazama ilihusishwa kama inavyoelezewa katika mhimili wa pili wa nadharia ya Bruner (Roya na Hanieh, 2015). Hata hivyo, Nelima (2012), anayapinga matokeo haya anaposema kuwa walimu hutumia mbinu ya mhadhara pekee katika ufundishaji wao.

Nayo asilimia 28.57 (N=2) ya walimu saba waliohojiwa ilitumia tarakilishi kufundisha vielezi. Walimu hawa walikubali kuwa wao hutumia mtandao kwenye tarakilishi kupata majarida yenye sentensi mbalimbali zilizo na vielezi. Sentensi hizi hutumiwa darasani kufundisha aina mbali mbali za vielezi.

Matokeo yalibaini kuwa asilimia 28.57 (N=2) ya walimu waliohojiwa ilitumia tarakilishi kufundisha mada ya sarufi ya uakifishaji. Walimu hawa walitumia hotuba ambazo wamezikagua na kuhakikisha kuwa zinazingatia kanuni za kisarufi kufundishia matumizi ya alama za uakifishaji za kikomo na kipumuo. Matumizi ya tarakilishi kufundishia uakifishaji huwashirikisha wanafunzi ipasavyo. Kama asemavyo Bruner (Christie, 2005), ufundishaji si kuhamisha maarifa tu kutoka kwa mwalimu hadi kwa mwanafunzi bali huhusisha jinsi mwanafunzi anashirikishwa katika mchakato huu. Hili liliweza kudhihirika kupitia kwa matumizi ya tarakilishi kufundishia kipengele cha uakifishaji.

Matokeo ya utafiti yalithibitisha kuwa, asilimia 14.29 (N=1) ya walimu saba ilitumia tarakilishi kufundisha muundo wa sentensi. Mwalimu huyu alitufahamisha kuwa, yeye hutumia mtandao kwenye tarakilishi kupata majarida yenye sentensi mbali mbali. Majarida haya hutumiwa darasani kufundisha muundo wa sentensi. Aidha, asilimia 14.29 (N=1) ilitumia tarakilishi kufundisha kipengele cha nyakati na hali. Asilimia hii ni finyu

kutokana na changamoto ya upungufu wa muda wa matayarisho ya kutumia tarakilishi katika ufundishaji. Changamoto hii inaoana na changamoto za matokeo ya utafiti wa Kariuki (2017), ambaye aligundua kuwa, walimu katika kaunti ya Nyandarua walikumbwa na upungufu wa muda wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa matumizi ya tarakilishi katika kufundisha na kujifunza sarufi ni finyu mno. Kwa hivyo, walimu na wanafunzi hawapati matokeo bora ya ufundishaji na ujifunzaji. Habari hizi zinaakisi maoni ya Njoroge (2014), anayesema kuwa, wanafunzi hupata changamoto tele katika kipengele cha sarufi kwa kuwa mbinu bunifu hazitumiwi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Tarakilishi ni kifaa cha kisasa ambacho kinapaswa kutumiwa shuleni. Kifaa hiki huwa na sehemu ya kutumia santuri vilivyorekodiwa sauti na picha za vitu husika kulingana na mada ya somo. Kwa hivyo, kwa kutumia santuri kwa tarakilishi, mwanafunzi huielewa mada hiyo kwa urahisi. Matokeo ya hali hii ni kuwa mwanafunzi huielewa mada hiyo kwa urahisi kutokana na kuona anachofundishwa kama inavyoelezewa katika mhimili wa pili wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi Bruner (Marzano, 2011). Hata hivyo, matokeo haya ni kinyume na matokeo ya Abuli (2013) anayesema kuwa, vifaa vya kisasa havitumiki katika ufundishaji na ujifunzaji katika shule za upili. Anasema kuwa, ukosefu wa matumizi ya vifaa vya kisasa huchangia matokeo duni ya ufunzaji wa masomo yote.

### 4.3.2 Jinsi Wanafunzi hutumia Tarakilishi Kujifunza

Mtafiti alichunguza jinsi wanafunzi hutumia tarakilishi kujifunza. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.4: Jinsi Wanafunzi hutumia Tarakilishi Kujifunza**

| Matumizi | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| Kufanya utafiti wa sarufi mtandaoni | 05 | 4.76% |
| Kuhifadhi nukuu za sarufi | 06 | 5.71% |
| Kutazama mchezo wa kandanda | 22 | 20.95% |
| Kucheza mchezo wa kamari | 14 | 13.33% |
| Kutazama filamu | 18 | 17.14% |
| Kuwasiliana na marafiki mtandaoni | 20 | 19.05% |
| Kuhifadhi na kutazama muziki | 15 | 14.29% |
| Kutafuta maswali ya marudio mtandaoni | 05 | 4.76% |
| **Jumla** | **105** | **100** |

Kwa mujibu wa matokeo katika jedwali 4.4, asilimia 4.76 (N=5) ya wanafunzi mia moja na watano waliohojiwa ilitumia tarakilishi kufanya utafiti wa kimasomo. Nayo asilimia 5.71 (N=6) ya wanafunzi hawa ilitumia tarakilishi kuhifadhi nukuu. Aidha, asilimia 20.95 (N=22) ya wanafunzi ilitumia tarakilishi kutazama mchezo wa kandanda. Isitoshe, asilimia 13.33 (N=14) ya wanafunzi waliohojiwa ilitumia tarakilishi kucheza mchezo wa kamari. Vile vile, asilimia 17.14 (N=18) ya wanafunzi mia moja na watano ilitumia tarakilishi kutazama filamu. Asilimia 19.05 (N=20) ilitumia tarakilishi kuwasiliana na marafiki huku asilimia 14.29 (N=15) ikitumia tarakilishi kuhifadhi na kutazama muziki. Kwa upande mwingine, asilimia 4.76 (N=5) ilitumia tarakilishi kutafuta maswali ya marudio mtandaoni.

Kutokana na matokeo haya, ni wazi kuwa, asilimia ndogo 15.23 (N=16) ya wanafunzi, wanatumia tarakilishi katika shughuli za masomo. Asilimia 84.76 (N=89) ya wanafunzi ilitumia tarakilishi kutazama michezo ya kandanda, kucheza michezo ya kamari, kkutazama filamu, kuwasiliana na marafiki mtandaoni na kuhifadhi na kutazama muziki. Matokeo haya yanaoana na matokeo ya Abuyeka (2014) anayesema kuwa, wanafunzi wanafaa kutumia mtandao kwenye tarakilishi ipasavyo ili kuinua viwango vyao vya ujifunzaji bali wasivivutimie katika mambo yasiyo ya kielimu.

### 4.3.3 Jinsi Walimu hutumia Vipakatalishi Vinapounganishwa na Vinuruweo Kufundisha Vipengele vya Sarufi

Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2013), kinuruweo ni kifaa ambacho kinaweza kutumiwa na mwalimu kufundisha. Katika mbinu hii kipakatalishi hutumiwa pamoja na kinuruweo kurusha mwanga kwenye ubao mweupe. Mwanga huo unaweza kurusha maneno, majedwali au picha. Mwalimu huandaa nukuu, michoro, majedwali pamoja na picha kwa kutumia kipakatalishi. Kinuruweo humsaidia mwalimu kurusha yote aliyoyaandaa kwa ajili ya wanafunzi kuandika au kusoma ili waweze kushiriki katika somo husika. Kama inavyojitokeza katika mhimili wa tatu wa nadharia ya kujifunza kiugunduzi yake Bruner (Roya na Hanieh, 2015) mwanafunzi hupata maarifa zaidi kwa kutazama badala ya kuambiwa na mwalimu. Utafiti ulitaka kuchunguza matumizi ya Vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika kufundisha vipengele mbalimbali vya sarufi. (Rejelea kiambatisho E). Matokeo yanadhihirishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.5: Jinsi Walimu hutumia Vipakatalishi Vikiunganishwa na Vinuruweo Kufundisha Vipengele vya Sarufi**

| Mada ya sarufi. | Matumizi ya vipakatalishi pamoja na vinuruweo. | Asilimia |
|---|---|---|
| Muundo wa sentensi | 2 | 25% |
| Nyakati na hali | 1 | 12.5% |
| Uakifishaji | 1 | 12.5% |
| Uchanganuzi wa sentensi | 1 | 12.5% |
| Usemi halisi na usemi wa taarifa | 2 | 25% |
| Vielezi | 1 | 12.5% |
| **Jumla** | **8** | **100%** |

Jedwali 4.5, linaonyesha matumizi ya vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo kufundisha sarufi katika kaunti ndogo ya Moiben. Vifaa hivi vinatumiwa kwa kiwango cha chini mno. Kati ya walimu 15 (100%) waliohusishwa katika utafiti, ni asilimia 53.33 (N=8) pekee ilikubali kutumia vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo kufundisha mada mbalimbali za sarufi. Asilimia 6.67 (N=1) ilitumia kipakatalishi na kinuruweo kufundisha kipengele cha sarufi cha nyakati na hali.

Lugha ya Kiswahili huwa na nyakati tatu ambazo huwakilishwa na viambishi mbalimbali. Kuna wakati uliopita, uliopo na ujao. Katika hali kuna hali timilifu, hali ya mazoea, masharti na hali isiyodhihirika. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, mwalimu huyu alitumia kinuruweo kurusha slaidi iliyovutia yenye na nyakati mbalimbali na viambishi vinavyowakilisha nyakati hizi kwenye ubao mweupe. Matumizi haya ya slaidi zenye kuvutia, yaliweza kuteka ari ya wanafunzi ya kutaka kujifunza zaidi kama inavyoelezewa katika mhimili wa tatu wa nadharia ya kujifunza kiugunduzi Bruner

(Hare, 2005). Hata hivyo, matokeo haya ni kinyume na matokeo Njogu na Nganje (2012) ambao walilalamikia jinsi walimu huchagua vifaa vya kufundishia Kiswahili kutokana na mielekeo yao hasi kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa.

**Jedwali 4.6: Matumizi ya Kipakatalishi na Kinuruweo Kufundisha Nyakati na Hali**

| **Nyakati** | **Hali** |
|---|---|
| Uliopita – ‘li’ | Timilifu – ‘me’ |
| Uliopo – ‘na’ | Mazoea – ‘Hu’ |
| Ujao- ‘ta’ | Masharti- ‘nge’ ‘ngeli’ ‘ngali |

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa, asilimia 12.5 (N=1) ya walimu ilitumia kinuruweo kuchanganua sentensi za Kiswahili. Asilimia hii ni ya chini mno kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi shuleni. Hali hii ilisababisha msongamano katika vyumba vya TEHAMA.

Alivyogundua Kamotho (2001), kwamba, idadi kubwa ya wanafunzi ina athari hasi katika matumizi ya vifaa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji, changamoto hii vile vile ilijitokeza katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Kutokana na agizo la serikali kwamba, wanafunzi wote wanafaa kujiunga na shule za upili baada ya kufanya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane, wanafunzi katika shule za upili wamekuwa wengi sana. Hali hii, imetatiza matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji .

Hatima ya uchanganuzi wa sentensi ni kubainisha aina za maneno yaliyotumika kujenga sentensi husika. Sentensi huchanganuliwa kwa kutumia mistari, jedwali na mchoro wa matawi. Mwalimu huyu alitufahamisha kuwa yeye hutumia kipakatalishi kuchanganua mifano ya sentensi kwa njia nne kuu; mistari, jedwali, mishale na mchoro wa matawi. Mifano hii ilihifadhiwa kwenye slaidi na hatimaye kurushwa kwenye ubao mweupe ili wanafunzi watazame. Njia ya mistari iliwekwa kwenye slaidi ya kwanza, mfano wa jedwali kwenye slaidi ya pili na mfano wa jedwali kwenye slaidi ya tatu. Hali hii ilisaidia ufafanuzi wa urahisi wa uchanganuzi wa sentensi. Vile vile, iliokoa muda kwa kuwa mwalimu hahitaji kuandika ubaoni

**Jedwali 4.7: Uchanganuzi wa Sentensi kwa Kutumia Mishale**

| | |
|---|---|
| Yeye na mkurugenzi mgeni walishangiliwa mkutanoni | |
| S →KN+KT | KT→T+E |
| KN→W+U+KN | T→walishangiliwa |
| W→yeye | E→mkutanoni |
| U→na | |
| KN→ N+V | |
| N→mkurugenzi | |
| V→mgeni | |

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, asilimia 25 (N=2) ya walimu ilitumia kipakatalishi pamoja na kinuruweo kufundisha usemi halisi na usemi wa taarifa. Usemi wa taarifa ni

ripoti kuhusu mambo yaliyosemwa. Katika usemi huu si lazima maneno yatokee kama yalivyotamkwa na msemaji. Yanaweza kubadilishwa lakini ni sharti ujumbe ubakie ule ule.

Walimu walikubali kuwa, wao hutumia vipakatalishi kupata semi faafu kwenye mtandao. Semi hizi huwa semi halisi na semi za taarifa. Baada ya kupata semi hizi kwenye mtandao, semi hizi huhifadhiwa kwenye kipakatalishi na baadaye kinuruweo hutumika kurusha semi hizi kwenye ubao mweupe. Mara nyingi semi za taarifa za habari hutumika. Matumizi haya yalithibitishwa kuwa faafu kwa kuwa wanafunzi hujifunza kwa kutazama kama unavyoelekeza mhimili wa tatu wa nadharia ya kujifunza kiugunduzi yake Bruner (Marzano 2011) kwamba wanafunzi hupata maarifa zaidi kwa kutazama. Hata hivyo, utafiti unashauri kuwa ni sharti walimu wawe makinifu wanapochagua semi za kufundishia. Ilibainika kuwa, hii ni mbinu bunifu ya kufundisha na kujifunza sarufi ambao huleta uchangamfu darasani kama anavyohoji Njoroge (2014).

Mfano wa usemi halisi

> **"*Wananchi wa Rwanda wameanza kupata utulivu baada ya vita vya miaka mingi,"* balozi wa Rwanda aliwaambia watu waliohudhuria sherehe hiyo**.

Huu ni mfano wa usemi halisi uliotolewa moja kwa moja mtandaoni na kurushwa kwenye ubao mweupe ili kutumika kama mfano wa usemi halisi.

Mfano wa usemi wa taarifa.

> ***Rais alipowasili kutoka Marekani aliwaambia waliomlaki kwamba Benki ya dunia imekubali kuipa Kenya mkopo wa shilingi bilioni hamsini*.**

Huu ni mfano wa usemi wa taarifa kama ilivyoripotiwa kwenye chombo cha habari. Usemi huu ulitumika kama mfano wa usemi wa taarifa.

Asilimia 12.5 (N=1) ya walimu ilitumia kipakatalishi pamoja na kinuruweo kufundisha uakifishaji. Asilimia hii ya 12.5 ilichangiwa na ukosefu wa mtandao shuleni. (Rejelea kiambatisho M). Kuakifisha ni kutumia alama za kuakifisha ipasavyo ili kuleta maana ikusudiwayo na hivyo kurahisisha mawasiliano. Kinuruweo kilitumika kurusha matumizi ya alama mbalimbali kwenye ubao mweupe. Matumizi haya ya vipakatalishi pamoja na vinuruweo huteka ari ya mwanafunzi ya kutaka kujua zaidi. Hali hii huwapa wanafunzi hamu ya kutaka kujifunza kama inavyojitokeza katika mhimili wa nne wa Bruner (Hill, 1999) kwamba ari ya mwanafunzi ya kutaka kujua zaidi inafaa kuchochewa na mwalimu. Matumizi haya yalionekana kuwa bora kinyume na madai ya Kariuki (2017), anayesema kwamba, shule nyingi zina upungufu wa vifaa vya kufundishia na walimu wengi hawavitumii.

Wakati huo huo matumizi ya vipakatalishi pamoja na vinuruweo huleta athari chanya ya kujifunza kwa kutazama. Hali hii humwezesha mwanafunzi kupata maarifa zaidi kwa kutazama. Kama asemavyo Bruner (Marzano, 2011), katika mhimili wa tatu kwamba mwanafunzi hupata maarifa zaidi kwa kutazama badala ya kuambiwa na mwalimu, ilibainika kuwa matumizi ya vipakatalishi vinapounganishwa na vinuruweo huleta athari hii ya kutazama.

**Jedwali 4.8: Mfano wa Slaidi ya Uakifishaji (Rejelea kiambatisho H na M)**

Matumizi ya nukta

- Mwishoni mwa sentensi
- Kuandika vifupisho
- Kuandika tarehe

### 4.3.4 Jinsi Wanafunzi hutumia Vipakatalishi Vikiunganishwa na Vinuruweo Kujifunza

Mtafiti alichunguza jinsi vipakatalishi na vinuruweo vinavyopatikana shuleni vinatumiwa na wanafunzi. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.9: Jinsi Wanafunzi hutumia Vipakatalishi pamoja na Vinuruweo Kujifunza**

| Matumizi | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Shughuli za masomo | 30 | 29% |
| Kurusha filamu nyakati za matumbuizo | 75 | 71% |
| **Jumla** | **105** | **100** |

Matokeo katika jedwali 4.9, yanaonyesha kuwa vipakatalishi pamoja na vinuruweo vinatumiwa zaidi na wanafunzi katika shughuli za matumbuizo. Asilimia 71 (N=75) ya wanafunzi ilikubali kutumia vipakatalishi na vinuruweo katika shughuli za matumbuizo.

Nayo asilimia 29 (N=30) ya wanafunzi waliohojiwa ilikiri kutumia vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika shughuli za masomo. Ni bayana kutokana na matokeo haya kwamba ingawa wanafunzi wanavitumia vipakatalishi, matumizi yao kwa manufaa ya masomo ni finyu. Hii ni kutokana na ukosefu wa ujuzi wa kuvitumia vifaa vya kisasa baina ya wanafunzi. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata ujuzi wa matumizi ya vifaa vya kisasa, wanapaswa kupewa fursa ya kuvitumia vifaa hivi katika shughuli za masomo kama asemavyo Makokha (2015).

Asilimia 29 (N=30) pekee ilivitumia katika shughuli za masomo. Hali hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hawadhamini vifaa vya kisasa katika kujifunza. Wengi wao wanavitumia vifaa hivi katika shughuli za kujiburudisha. Isitoshe, hali hii ilichangiwa na ukosefu wa muda wa kuvitumia vifaa hivi katika shughuli za masomo. Ili kulikabili tatizo hili wanafunzi wanapaswa kutengewa vipindi maalum vya kutumia tarakilishi na vipakatalishi katika shughuli za masomo kama anavyohoji Kareji (2016).

Kwa hivyo, pana haja ya kuwahamasisha wanafunzi kuhusu manufaa ya kutumia vifaa vya kisasa ili kuinua ujifunzaji.

**4.4 Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji wa Sarufi**

Mtafiti alihakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika kufundisha na kujifunza sarufi katika shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben. Matokeo ni kama yanavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.10: Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa Kufunza Sarufi**

| **Umuhimu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Hurahisisha uelewekaji | 15 | 100% |
| Huweka kumbukumbu ya yaliyofundishwa | 14 | 93.33% |
| Huchangia ubunifu | 12 | 80% |
| Huendeleza vipawa | 13 | 86.67% |
| Huboresha matokeo ya ufundishaji | 14 | 93.33% |
| Huleta uvutio wa somo | 15 | 100% |
| Huwapa motisha wanafunzi kushiriki katika somo | 15 | 100% |
| Huokoa muda wa kunakili hoja | 14 | 93.33% |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Kwa mujibu wa jedwali 4.10, matokeo ya utafiti yalithibitisha kuwa vifaa vya kisasa ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Asilimia 100 (N=15) ya walimu ilikubali kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huwapa wanafunzi motisha ya kushiriki katika somo la sarufi na kuwapa ari ya kutaka kujifunza zaidi. Matokeo haya yanasadikishwa na mhimili wa nne wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi ambayo inasisitiza kuwa, ari ya mwanafunzi ya kutaka kujifunza zaidi inapaswa kuchochewa na mwalimu Bruner (Hare, 2005). Isitoshe, matokeo haya yanaoana na maoni ya Too (1996), kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa huwashirikisha wanafunzi katika hatua zote za ufundishaji na ujifunzaji. Matumizi haya ya vifaa vya kisasa yalibainika kuwa bora vikitumika kufundisha sarufi ingawa Nelima (2012) anasema kuwa walimu hutumia mbinu ya mhadhara pekee katika ufundishaji wao

Asilimia 93.33 (N=14) ya walimu waliohojiwa ilikiri kuwa vifaa vya kisasa vya kufundishia sarufi huboresha matokeo ya ufundishaji. Kwa hivyo, ili kupata matokeo bora ni sharti ufundishaji na ujifunzaji uhusishe teknolojia ya kisasa kama anavyohoji Kimani (2015). Utafiti uliendelea kufichua kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa huendeleza vipawa vya wanafunzi. Asilimia 86.67 (N=13) ya walimu waliohojiwa, ilikubaliana na wazo hili. Vile vile, ilibainika kuwa, vifaa vya kisasa vya kufundishia sarufi huokoa muda wa mwalimu wa kunakili hoja ubaoni na hivyo kumfanya mwalimu kudhibiti kipindi ipasavyo. Asilimia 93.33 (N=14) ya walimu waliohojiwa ilishadidia hoja hili. Nayo asilimia 100 (N=15) ya walimu waliohojiwa ilikubali kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa hurahisisha uelewekaji wa somo la sarufi. Matokeo haya yanaoana na maoni ya Quist (2005), anaposema kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa hurahisisha uelewekaji wa somo.

Wakati huo huo, asilimia 93.33 (N=14) ya walimu waliohojiwa iliafiki kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huchangia kumbukumbu ya yaliyofundishwa kwa njia bora zaidi kama asemavyo Akung'u (2014). Isitoshe, asilimia 80 (N=12) ya walimu waliohojiwa, walikubali kuwa, vifaa vya kisasa huchangia ubunifu wa wanafunzi. Hatimaye, asilimia 100 (N=15) ilikubali kuwa vifaa vya kisasa huleta uvutio katika somo kama asemavyo Githinji (2016).

Matokeo haya yanaonyesha kuwa, matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumiwa pamoja na vinuruweo yana manufaa katika kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Hii inathibitisha kuwa, matumizi ya vifaa hivi katika ufundishaji na ujifunzaji ni muundo

bora wa kufundisha kama inavyojitokeza katika mhimili wa kwanza wa nadharia ya kujifunza kiugunduzi yake Bruner (Krashen, 1988).

### 4.4.1 Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa Kujifunza Sarufi

Mtafiti alichunguza umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ujifunzaji wa sarufi kwa mujibu wa wanafunzi. (Rejelea kiambatisho B). Matokeo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.11: Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa Kujifunza Sarufi**

| Matumizi | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Hurahisisha uelewekaji wa sarufi | 102 | 97.14% |
| Huleta uvutio katika somo la sarufi | 103 | 98.10% |
| Huleta uchangamfu katika ujifunzaji wa sarufi | 94 | 89.52% |
| Huweka kumbukumbu ya yaliyofundishwa | 92 | 87.62% |
| Huboresha matokeo ya ujifunzaji wa sarufi. | 96 | 91.43% |
| Huokoa muda wa kunakili hoja. | 102 | 97.14% |
| **Jumla** | **105** | **100** |

Kutokana na matokeo katika jedwali 4.11, asilimia 97.14 (N=102) ya wanafunzi mia mmoja na watano waliohojiwa ilikubali kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa hurahisisha uelewekaji wa sarufi. Matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinavyotumika pamoja na vinuruweo yana uwezo wa kukuza usomaji wa lugha na kuufanya uwe wa kusisimua na hivyo kurahisisha uelewekaji. Nayo asilimia 98.10 (N=103) ya wanafunzi waliohojiwa ilikiri kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huleta uvutio katika somo la sarufi. Vile vile, asilimia 89.52 (N=94) ya wanafunzi walithibitisha kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa

huleta uchangamfu katika ujifunzaji wa sarufi. Matokeo haya yanaoana na maoni ya Marine na Hilles (2008) wanaposema kuwa, vifaa vya kisasa ni muhimu sana katika somo la sarufi kwa kuwa husaidia kuhifadhi motisha katika somo kwa viwango vya juu.

Isitoshe, asilimia 87.62 (N=92) ya wanafunzi waliohojiwa ilikubali kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huchangia kumbukumbu za dhana zilizofundishwa kwa njia bora zaidi. Hisi ya kutazama na kusikiliza ikihusishwa katika ufundishaji na ujifunzaji, huchangia kumbukumbu za muda mrefu (Nunan, 2004). Aidha, asilimia 91.43 (N=96) Ilikiri kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa huboresha matokeo ya ujifunzaji wa sarufi. Matokeo haya yanaoana na maelezo ya Kipkoech (2017), kuwa, vifaa vinavyohusisha teknolojia ya kisasa vikitumika katika ujifunzaji, hurahisisha uelewekaji wa dhana.

Hatimaye, asilimia 97.14 (N=102) ya wanafunzi waliohojiwa ilikubali kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huokoa muda wao wa kunakili hoja muhimu. Habari hizi zinaakisi maoni ya Wanjala na Kavoi (2013), wanaposema kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa kama vile vipakatalishi vikitumika pamoja vinuruweo humwepushia mwalimu muda mwingi wa kuandika ubaoni hivyo kuokoa muda na kumwezesha mwalimu kufundisha mambo mengi sana ndani ya muda mfupi.

Ni bayana kuwa, vifaa vya kisasa huleta athari ya kujifunza kwa kutazama. Kutokana na hali hii, hunasa hisia za mwanafunzi na kurahisisha uelewekaji wa somo kama inavyoelekezwa na mhimili wa tatu wa nadharia ya kujifunza kiugunduzi ambao unasisitiza kuwa mwanafunzi hupata maarifa zaidi kwa kutazama badala ya kuambiwa na mwalimu Bruner (Christie, 2005).

## 4.5 Hitimisho

Katika sura hii, utafiti umewasilisha na kuchanganua data ya hali halisi kuhusu matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Katika kuafiki matumizi haya, utafiti umeangazia yafuatayo: Kwanza, kuthibitisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa. Pili, kuchunguza jinsi walimu na wanafunzi hutumia tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Tatu, sura hii imeangazia umuhimu wa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Sura inayofuata imeshughulikia muhtasari wa utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya tafiti za ziada.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Tasnifu hii ililenga kutathmini matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Vifaa mahususi vilikuwa matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika na vinuruweo. Katika sura hii, utafiti umeshughulikia muhtasari wa tasnifu hii. Isitoshe, umeshughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti kuhusu matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Sura hii vile vile imeshughulikia matatizo yaliyojitokeza wakati wa utafiti, mapendekezo ya utafiti wenyewe na mapendekezo ya tafiti zaidi.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Ulilenga vifaa mahususi ambavyo ni matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika na vinuruweo. Utafiti ulichochewa na mabadiliko katika sekta ya elimu ambayo yanamhitaji mwalimu kuhusisha usasa katika ufundishaji na ujifunzaji wake.

Katika sura ya kwanza, utafiti umeshughulikia usuli wa mada ya utafiti na suala la utafiti. Vile vile, sura hii imeshughulikia malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Sababu za kuichagua mada pia zimedhihirishwa katika sura hii. Aidha, sura hii imeangazia upeo na mipaka ya utafiti, umuhimu wa utafiti na nadharia ya utafiti.

Nayo sura ya pili imeshughulikia tahakiki ya maandishi . Katika kuhakiki maandishi, utafiti ulizingatia yafuatayo: mbinu za ufundishaji wa sarufi, matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji, aina za vifaa vya kisasa vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji, matumizi bora ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji, umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na changamoto za matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji.

Sura ya tatu imeshughulikia muundo wa utafiti. Hapa, sababu za kuchagua eneo la utafiti zimedhihirishwa. Isitoshe, mbinu za usampulishaji zimeorodheshwa. Aidha, utafiti umefafanua njia za kukusanya data ambazo ni: uchunzaji darasani, ujazaji wa hojaji na mahojiano. Wakati huo huo, vifaa vya kukusanyia data ambavyo ni mwongozo wa uchunzaji, hojaji na mwongozo wa mahojiano vimejadiliwa. Isitoshe, sura hii imeshughulikia utafiti mwigo, unukuzi wa data na uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Hatimaye, imebainisha maadili yaliyozingatiwa katika utafiti.

Matokeo ya utafiti yamejadiliwa katika sura ya nne. Utafiti umethibitisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Wakati huo huo, sura hii imejadili jinsi walimu na wanafunzi hutumia tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Aidha, sehemu hii imehakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben. Hatimaye, imetathmini changamoto zinazokumba matumizi ya vifaa hivi..

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameweza kujadiliwa chini ya kila mojawapo ya malengo ya utafiti kama ifuatavyo:

### 5.3.1 Upatikanaji wa Vifaa vya Kisasa vya Ufundishaji na Ujifunzaji

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kuthibitisha vifaa vya kisasa vya ufundishaji vinavyopatikana katika kaunti ndogo ya Moiben. Kati ya shule kumi na tano zilizolengwa na utafiti, ilibainika kuwa asilimia 46.67 (N=7) ilikuwa na vyumba vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kwa jumla, tarakilishi nane zilipatikana huku vipakatalishi tisa vikipatikana katika shule za upili zilizolengwa na utafiti.

Shule ambazo zilikuwa na vyumba vya TEHAMA ni shule ya wasichana ya Moi, shule ya upili ya Kimumu, shule ya upili ya Eldoret ya kati, shule ya upili ya Chuo Kikuu cha Eldoret, shule ya upili ya Itigo na shule ya upili ya Kuinet. Vyumba hivi vilikuwa na vinuruweo ambavyo vilitumika pamoja na vipakatalishi kufundisha. Vipakatalishi pamoja na vinuruweo vilitumika vilitumika kurusha maandishi kwenye ubao mweupe. Aidha, vilitumika kurusha picha na video ambazo ziliwasaidia wanafunzi kulielewa somo la sarufi kupitia uwezo wa kuona na kusikia.

Kando na vifaa vya kisasa, utafiti huu ulitaka kuthibitisha vifaa vinavyotumiwa mara nyingi na walimu katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Ilibainika kuwa ubao na chati vilipatikana katika shule zote zilizolengwa na utafiti.Vifaa hivi vilitumika kama vifaa vikuu vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi. Asilimia 100 (N=15) walitumia ubao kama kifaa kikuu cha ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi huku asilimia 100 (N=15) wakitumia chati kufundishia sarufi. Matokeo haya yalishabihiana na matokeo ya Wambui

(2017), ambaye katika utafiti wake alibaini kuwa walimu wengi walitumia chati kama kifaa kikuu katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 5.3.2 Jinsi Vifaa vya Kisasa Vinatumika Kufundisha na Kujifunza Sarufi

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi walimu hutumia vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika kaunti ndogo ya Moiben. Vifaa hivi ni, matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumika pamoja na vinuruweo. Katika kuchunguza ufundishaji wa sarufi, utafiti ulilenga mada za sarufi ambazo ni: usemi halisi na usemi wa taarifa, uchanganuzi wa sentensi, vielezi, uakifishaji, muundo wa sentensi na nyakati na hali.

Utafiti ulifichua kuwa, asilimia 14.29 (N=1) ya walimu waliohojiwa ilitumia tarakilishi kufundisha kipengele cha sarufi cha usemi halisi na usemi wa taarifa huku asilimia 28.57 (N=2) ikitumia tarakilishi kufundisha vielezi. Aidha, asilimia 28.57 (N=2) ya walimu hawa ilitumia tarakilishi kufundisha uakifishaji. Wakati huo huo asilimia 14.29 (N=1) ya walimu waliohojiwa ilitumia tarakilishi kufundisha kipengele cha nyakati na hali.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa matumizi ya tarakilishi kufundisha sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben ni finyu mno. Tarakilishi ni kifaa cha kisasa ambacho kinapaswa kutumiwa shuleni. Kifaa hiki huwa na sehemu ya kutumia santuri vilivyorekodiwa sauti, maandishi na picha za vitu husika kulingana na mada ya somo. Kwa hivyo, matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji wa sarufi huwafanya wanafunzi kuelewa mada husika kwa urahisi. Matokeo ya hali hii ni kuwa mwanafunzi huilewa mada hiyo kwa urahisi kutokana na kuona anachofundishwa kama inavyoelezewa katika mhimili wa pili wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi Bruner ( Marzano, 2011).

Aidha, utafiti ulichunguza jinsi wanafunzi hutumia tarakilishi. Matokeo yalionyesha kuwa, baina ya wanafunzi, tarakilishi inatumika katika viwango vya chini mno katika shughuli za masomo. Asilimia 84.76 (N=89) ya wanafunzi ilitumia tarakilishi kutazama michezo ya kandanda, kucheza michezo ya kamari, kutazama filamu, kuwasiliana na marafiki mtandaoni na kuhifadhi na kutazama muziki. Asilimia 10.48 (N=16) pekee ilitumia tarakilishi katika shughuli za masomo.

Vile vile, utafiti ulichunguza matumizi ya vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo. Vifaa hivi vilitumiwa kwa viwango vya chini mno kufundisha sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Kati ya walimu 15 (100%) waliohusishwa katika utafiti, ni asilimia 53.33 (N=8) pekee ilitumia vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo kufundisha mada mbalimbali za sarufi. Asilimia 25 (N=2) ya walimu walitumia vipakatalishi vilivyounganishwa na vinuruweo kufundisha muundo wa sentensi na usemi halisi na usemi wa taarifa huku asilimia 12.5 (N=1) ikitumia vifaa hivi kufundisha nyakati na hali, uakifishaji, vielezi na uchanganuzi wa sentensi.

Isitoshe, utafiti ulitaka kujua jinsi vipakatalishi na vinuruweo vinavyopatikana shuleni hutumiwa na wanafunzi. Matokeo yanaonyesha kuwa vipakatalishi pamoja na vinuruweo vinatumiwa zaidi na wanafunzi katika shughuli za matumbuizo. Asilimia 71 (N=75) ya wanafunzi ilikubali kutumia vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika shughuli za matumbuizo. Nayo asilimia 29 (N=30) ya wanafunzi waliohojiwa ilikiri kutumia vipakatalishi pamoja na vinuruweo katika shughuli za masomo. Ni bayana kutokana na matokeo haya kwamba ingawa wanafunzi wanavitumia vipakatalishi, matumizi yao katika shughuli za masomo ni finyu mno.

### 5.3.3 Umuhimu wa Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi

Lengo la tatu la utafiti lilikuwa kuhakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Matokeo ya utafiti yalithibitisha kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi.

Asilimia 100 (N=15) ya walimu waliohojiwa ilikiri kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa hurahisisha uelewekaji wa somo la sarufi huku asilimia 93.33 (N=14) ikikubali kuwa matumizi haya huweka kumbukumbu ya yaliyofundishwa kwa njia bora zaidi. Aidha, asilimia 80 (N=12) ya walimu waliohojiwa ilithibitisha kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huchangia ubunifu wa wanafunzi. Wakati huo huo, asilimia 93.33 (N=14) ya walimu hawa ilikubali kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji huboresha matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Nayo asilimia 100 (N=15) ya walimu ilikiri kuwa vifaa vya kisasa vya ufundishaji huleta uvutio katika somo la sarufi huku asilimia 100 (N=15) ikithibitisha kuwa vifaa hivi huwapa wanafunzi motisha ya kushiriki katika somo. Hatimaye, asilimia 93.33 (N=14) ya walimu waliohojiwa ilikubali kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji huokoaa muda wa mwalimu wa kunakili hoja ubaoni.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa, matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi ambavyo hutumiwa pamoja na vinuruweo yana manufaa katika kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Hii inathibitisha kuwa, matumizi ya vifaa hivi katika ufundishaji na ujifunzaji ni muundo bora

wa kufundisha kama inavyoelezwa katika mhimili wa kwanza wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi yake Bruner (Roya na Hanieh, 2015).

Wanafunzi vile vile walithibitisha kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu sana katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Asilimia 97.14 (N=102) ya wanafunzi waliohojiwa ilikiri kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa katika ujifunzaji hurahisisha uelewekaji wa sarufi huku asilimia 98.10 (N=103) wakithibitisha kuwa matumizi haya huleta uvutio katika somo la sarufi. Nayo asilimia 89.52 (N=94) ya wanafunzi ilikubali kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huleta uchangamfu katika ujifunzaji wa sarufi.

Kwa upande mwingine, asilimia 87.62 (N=92) ya wanafunzi ilithibitisha kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji huweka kumbukumbu ya yaliyofundishwa. Aidha, asilimia 91.43 (N=96) ya wanafunzi hawa walikiri kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji huboresha matokeo ya ujifunzaji wa sarufi huku asilimia 97.14 (N=102) ikikubali kuwa vifaa hivi huokoa muda wa kunakili hoja.

Kutokana na matokeo haya ni bayana kuwa, matumizi ya vifaa vya kisasa ni muhimu katika kuinua viwango vya ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben. Umuhimu huu unatokana na athari ya kutazama inayochangiwa na matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji kama inavyoangaziwa katika mhimili wa tatu wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi yake Bruner (Hare, 2005).

## 5.4 Hitimisho

Mada ya tasnifu hii ilikuwa ni matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili za kaunti ndogo ya Moiben, Uasin Gishu. Malengo ya utafiti yalikuwa: kuthibitisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa, kuchunguza jinsi walimu na wanafunzi walitumia vifaa vya kisasa, kuhakiki umuhimu wa matumizi ya vifaa hivi na kutathmini changamoto zinazowakumba katika matumizi ya vifaa vya kisasa.

Sababu ya kuchagua mada ya sarufi ilitokana na matokeo ya watafiti wa awali ambao walithibitisha kuwa kuna tatizo katika ufundishaji wa sarufi. Mtafiti alitaka kubaini iwapo matumizi ya vifaa vinavyohusisha teknolojia ya kisasa yanaweza kulitatua tatizo hili. Mtafiti alilenga matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo kama vifaa mahususi.

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa kuna matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili za kaunti ndogo ya Moiben japo kwa viwango vya chini mno. Vile vile, mtafiti alithibitisha kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa huweza kuinua matokeo ya ufundishaji wa sarufi. Kwa hivyo, walimu wanapaswa kutilia makazo wa matumizi yazo ili kuondoa ukavu katika ufunzaji wa vipindi vya sarufi.

## 5.5 Mapendekezo Kutokana na Utafiti

Mapendekezo yanayowasilishwa hapa yanatokana na matokeo ya utafiti huu na yanalenga kuchangia katika kuimarisha matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji. Mapendekezo hayo ni:

Serikali iwaandalie walimu wa Kiswahili katika kaunti ndogo ya Moiben warsha na semina ili wapate maarifa na ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa. Kwa kufanya hivi, serikali itaondoa changamoto ya ukosefu wa ujuzi miongoni mwa walimu wanaofundisha sarufi.

Serikali ya kitaifa inapaswa ipunguze ushuru wa kuvinunua tarakilishi na vipakatalishi pamoja na vinuruweo ili kuhakikisha kwamba walimu na wanafunzi wanapata fursa kuvinunua kwa bei nafuu. Kwa kufanya hivi, vifaa vya kisasa vitapatikana katika kila shule. Hali hii itaondoa changamoto ya ukosefu wa fedha za kuvinunua vifaa hivi kama ilivyothibitisha matokeo ya utafiti.

Ushirikiano wa walimu, serikali ya kaunti ya Uasin Gishu, wanafunzi na wahisani wengine wa sekta elimu katika kuvinunua vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji . Kwa kufanya hivi, idadi ya shule zilizo na vyumba vya TEHAMA katika kaunti ndogo ya Moiben itaongezeka.

Utafiti vile vile unapendekeza kuanzishwa kwa maktaba ya vifaa vya kisasa vya kufundisha na kujifunza katika shule za sekondari katika kaunti ndogo ya Moiben. Kwa kufanya hivi vifaa hivi vya kisasa vitapatikana kwa urahisi kwa walimu wote na hivi vitatumika mara kwa mara.

Serikali ya kitaifa kupitia Wizara ya Elimu iweze kubuni kamati maalum ya kuwahamasisha walimu na wanafunzi kote nchini kuhusu matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji.

Vyuo vikuu vinafaa kutilia maanani matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji wanawapowatayarisha walimu kuenda nyanjani. Wahadhiri wanaowatahini walimu

wakati wa mazoezi ya ufundishaji watilie mkazo matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 5.6 Mapendekezo kuhusu Tafiti za Baadaye

Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika pamoja na vinuruweo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Moiben. Zifuatazo ni tafiti zaidi zinazoweza kufanywa:

Matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa vipengele vingine vya lugha ya Kiswahili kama vile:Matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji katika kufundisha fasihi andishi ya Kiswahili, matumizi ya vifaa vya kisasa vya ufundishaji na ujifunzaji katika kufundisha isimu jamii ya Kiswahili.

Utafiti kama huu vile vile, unaweza ukafanyika katika kiwango cha shule za msingi maanake vifaa vya kisasa kama vile vipakatalishi vilivyotolewa na serikali vinapatikana katika shule za msingi.

Pana haja ya kutafiti kuhusu sera za ukaguzi na matumizi wa vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuboresha matumizi ya vifaa hivi.

## MAREJELEO


Abuli, W.O (2013). *An Evaluation of the extent to which Audio, Visual and Audio-visual Media are used for Instruction. A case study of Lusengeli Secondary school in Vihiga County, Western Region, Kenya*. Maseno:Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno, Haijachapishwa.

Abuyeka, M. (2014). *Intergration of Information and Communication Technology in Teaching and Learning in Secondary Schools in Kakamega County.* Nairobi. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa

Aggarwal, J.C.(1995). *Essentials of Educational Technology; Teacing and Learning Innovations in Education.*New Delhi: Vikas Publishing House.

Akung'u, J. (2014). *Influence of Teaching and Learning Resources on Student Performance in Kenya Certificate of Secondary Education in Free Day Secondary Schools in Kenya*. Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Achilah, A. (2010). *Matumizi ya Mbinu ya Kimuktadha katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili katika Shule za Upili za Wilaya ya Kakamega*. Kakamega: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Haijachapishwa.

Ambuko, F. (2013). *Selection and use of Media in Teaching Kiswahili Language in Secondary Schools in Emuhaya District*. Kakamega:Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Bondo, Haijachapishwa.

Anol, B. (2012). *Social Science Research: Principles, Methods and Practices.*Florida: Creative Commons Attribution Publishers

Ary, D. (1972). *Introduction to Researching in Education*. New York: Holtrine.

Borg, H, & Gall, K. (1999). *Educational Research*. New York: Longman Publishers.

Bruner, J. (1966). *The Discovery Learning Theory*. New York: Cambridge University Press.

Bruner, J. (1990). *Acts of Meaning*.Cambridge, MA: Hardvard University Press

Oke, F.,E. & Brown, R., N. (2006). *Curriculum and Instruction*: *An introduction to Methods of Teaching*. London: London Publishers.

Casley, D., & Lury, D. (1981). *Data Collection in Developing Countries*. Oxford: Clarendon press.

Christie, A. (2005). *Constructivism and its Implications for Educators.* New York: Teachers College Press.

Creswell, J. (2014). *Research Design*. London. Sage Publishers.

Dale, E. (1969). *Professional*: *Theory into Practice. Vol 9*

Dorr, A. (1984). *The Teaching Face of Television*. New York: Brace Jovanovich Publishers.

D.F.I.D. (2009). *Department for International Development. Educational Leadership*, 30(42), 24-26

Enon, C. (1998). *Education Research and Measurement.* Kampala: Makerere University Publishers.

Eshiwani, G. (1988). *Science and mathematics education in Kenya*. Nairobi: Kenyatta University.

Gathumbi.,A & Ssebbunga, M. (2005). *Principles and Techniques of Language Teaching*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Githinji, M. (2016). *School Factors Influencing Instruction of Kiswahili Grammar in Public Secondary Schools in Baringo Central sub County*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa.

Grove, M. (2008). *Remedial Education in Primary School*. Pretoria: Haum Educational Publishers.

Gweyi, M. (2014). *Research Methods*. Nairobi: Co operative University Publishers.

Hare, D. (2005). Enhancing Technology Use In Student Teaching. *Journal of Technology and Teacher Education, 13(4)*

Hill, J. (1999). *Collocation Competence.* Massachusettes: Allyn & Bacon publishers.

Johnson, K. (1995). *Understanding Communication in Second Language Classroom*. New york : Cambridge University Press.

Kamotho, H. (2001). *Factors affecting Use of Instructional Materials in Secondary Schools of Muranga District*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa.

Kareji, F. (2016). *Factors influencing Board of Management's Governance of Information and Communication Technology in Public Secondary schools in Kapseret Division, Uasin Gishu*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

Kariuki, P. (2017). *Matumizi ya Nyenzo katika Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za Msingi, Jimbo la Nyandarua*. Nyandarua: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maasai Mara, Haijachapishwa.

Kawoya, V. (2012). The case for Kiswahili as a regional broadcasting language in East Africa, *The Journal of Pan African Studies*.

K.I.C.D, (2012). *Basic Education Framework. Use of Instructional Materials*. 45(3), 56 -57

Kimani, J. (2015). *Uhusiano wa Mbinu za Kufundishia Sarufi na Umilisi wa Mazungumzo ya Wanafunzi wa Sekondari, Kaunti Ndogo ya Thika Magharibi, Kenya*. Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

King'ei, K. (2007). *Changamoto za Sheng Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Kipkoech, T. (2017). *Effective Use of Digital Devices in Teaching and Learning of Christian Religious Education in Kericho County*. Kericho:Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kabianga, Haijachapishwa.

K.I.E, (2006). *Provision of Teaching and Learning Aids to Schools.* 38(41), 12-15

Kombo, D., & Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Wring.* Nairobi: Acts press.

Koross, R., & Murunga, F. (2017). *Mbinu za Kufundishia Kiswahili katika K21*. Eldoret. Utafiti foundation.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques.* New Delhi: Newage International Publishers.

Krashen, S. (1988). *Second Language Acquisition and Second Language Learning* London: Prentice Hall publishers.

Luvisia, C. (2003). *Study of Availability and use of Instructional Resources in the Teaching and learning of Kiswahili Grammar in Bungoma District*. Bungoma: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa

Magare, D. (2017). *Matumizi ya Majadiliano ya Makundi katika Kufunza Stadi ya Kuzungumza katika Tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Makokha, R. (2015). *The utilization of Instructional Resources in Teaching Kiswahili Poetry in Secondary schools in Nandi North District*. Eldoret:Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa.

Marine, C., & Hilles, S. (2008). *Techniques and Resources in Teaching Grammar*. Oxford: Oxford University Press.

Marzano, J. (2011). *Discovery-Based Instruction*. Cambridge: Harvard UniversityPress.

Mathooko, M. (2007). *Academic and Proposal Writing*.Nakuru: Amu Press

Mdee, J., Njogu, N. & Shafi, A. (2014). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mogeni, J. (2005). *Factors Influencing Utilization of Resources in Teaching Kiswahili in Selected Public Secondary Schools in Transmara District, Kenya* .Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa

Mugenda, O., & Mugenda A. (1999). *Research Methods.Qualitative and Quantitative Approaches.* Nairobi: Acts press.

Mligo, E. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantik*i. Dar es Salaam: Ecumenical Publishers.

Nelima, R. (2012). *Uchunguzi wa Mbinu za Kufundishia Hadithi Fupi katika Shule za Sekondari Wilayani Kakamega*. Kakamega: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Haijachapishwa

Nunan, D. (2004). *Task-Based Language Teaching*. Cambridge: Macmillan Publishers.

Ngonga, B. (2002). *An Assessment of English language Teacher Education in the Light of Classroom Needs: A case study of Maseno University*. Kisumu: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno, Haijachapishwa

Njogu, K. & Nganje, D. (2012) *Kiswahili kwa Vyuo vy Ualimu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, H. (2014). *Application of Songs in Teaching Kiswahili Grammar*. Nyandarua: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Karatina, Haijachapishwa.

Odera, F. (2007). *School Radio Programmes: A Case Study of Its Use in Selected Institutions in Nyanza Region in Kenya*. Great Britain: Wales Publishers.

Ogero, A. (2012). *Institution Based Factors Influencing Students Performance in Kiswahili at K.C.S.E in Sameta Division, Kisii County*.Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Oginga, O. (2010). *Matumizi ya Nyenzo katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi katika Shule za Secondary Wilayani Mumias na Matungu katika kaunti ya Kakamega*. Kakamega: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Haijachapishwa

Okwako, R. (1994). *A survey of Resources available for Teaching Reading in English in Secondary schools in Kenya.* Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa.

Onwonga, M. (2014). *Perception of teachers on the role of learning aids in teaching of English in Starehe Sub county*. Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oldham. C. (2012). *Resources from the Oldham County School Media Centre LMS.* Retrieved from http://www.ala.org/booklist.

Onen, D. (2005). *A General Guide to Research Proposal and Report*. Oxford: Oxford university press.

Onyango, O. (2009). *Matumizi ya Nyenzo katika Ufunzaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Madarasa ya Mwanzo ya Shule za Msingi za Manispaa ya*

*Kakamega*.Kakamega:Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia ya Masinde Muliro, Haijachapishwa

Ornstein, P. (1990). North *The effect ot Teachers Memory-Revelant Language on Children Strategy Use and Knowledge.* University of Carolina: Greens Publishers.

Parpert, T. (1987) *E-Tools for Teaching and Learning*. New Jersey: Pearson Publishers

Peil, M. (1995). *Social science Research Methods, A Handbook for Africa*(Second Revised Edition).Nairobi: East African Educational Publishers

Quist, D. (2006). *Primary Teaching Methods*. London: Macmillan publishers.

Robinson, W. (1980). *Learning Modules: A Concept for Extension Educators*. London: Houston College Publishers

Roya, G. & Hanieh, F. (2015). *New Implications for Instructional Technology*. New York. Norton Publishers

Sharman, D. (1983). *Research Methods in Social Science.* New Delhi: Sterling Publishers.

Skinner, B. (2003). *Verbal Behaviour*. New york: Appleton Publishers

Too, G. (1996). *Availability and use of Media in the Teaching of Mathematics: A survey of Nandi North District*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa

Trochim, W. (2002). *Research Design in Quantitative Methods.* New York: Mcgraw Hill Publishers.

Wambui, K. (2015). *Tathmini ya Matumizi ya Vifaa vya Kufundishia Msamiati wa Kiswahili katika Shule za Msingi za Umma, Kaunti ya Kisumu Mashariki Kenya*. Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Haijachapishwa.

Wanjala, F., & Kavoi, M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili kwa Wanafunzi, Walifunzi na Walimu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Walker, L. (1999). *Using Learning Resources to Enhance Teaching and Learning*. London: Longman Publishers

Wringe, C. (1995). *The Effective Teaching of Modern Teaching Languages.* UK: Longman Group Publishers.

Zacharia, S. (2012). *Instructional Materials in Teaching and Learning in Secondary Schools of Nyandarua District*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Haijachapishwa.

## KIAMBATISHO A: HOJAJI KWA MWALIMU

**KIAMBATISHO A: HOJAJI KWA MWALIMU**

Mimi ni Melly Kipchirchir Joachim, mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Nimetayarisha hojaji hii kutafiti kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za upili. Nakuomba utenge muda wa kujibu maswali ya hojaji hii. Ninaahidi kwamba habari zote utakazotoa zitahifadhiwa kwa siri wakati na baada ya utafiti huu.

**Maagizo**

Nakuomba uweke kikwaju katika visanduku ulivyopewa. Pale ambapo unahitajika kufafanua jibu lako, nakuomba utenge muda wa kuelezea jibu lako kwa kina.

1 Jinsia yako kiume [ ] kike [✓]

2. Kiwango chako cha elimu.

| | |
|---|---|
| Diploma | ✓ |
| Digrii | |
| Uzamili | |
| Uzamifu | |

3.Una tajriba ya miaka mingapi katika kufundisha Kiswahili?


| | |
|---|---|
| Miaka 0-5 | |
| Miaka 6-10 | ✓ |
| Miaka 11-15 | |
| Miaka 16-20 | |
| Zaidi ya miaka 20 | |

4.Unafunza vipindi vingapi vya sarufi kwa wiki?

| | |
|---|---|
| Kimoja | |
| Viwili | |
| Vitatu | |
| Vinne | |
| Vitano | |
| Sita | ✓ |

5.Unatumia vifaa vyovyote kufundisha sarufi?

Ndio [✓] La [ ]



6.Unatumia kifaa zaidi ya kimoja?

Ndio ☑ La ☐

Iwapo ni ndio, kwa nini?

Vifaa vya kufundishia kufidiana.

Iwapo ni la, kwa nini?

a) Tarakilishi Ndio ✓ La

Iwapo ni ndio unatumia kufundisha kipengele kipi cha sarufi?

Uchanganuzi wa sentensi ……………………

……

……………………………………………………

……

b) Vipakatalishi pamoja na vinuruweo Ndio ☑ La ☐

Iwapo ni ndio, unatumiaje?…………………………………………

Kuwapa wanafunzi fursa ……
Kufundishwa kwa kutazama (slides) ……………………

……

Unatumia vifaa hivi kufundisha vipengele gani vya sarufi?

Muundo wa sentensi. ……………………

……………………………………………………

……

8.Matumizi ya tarakilishi na vipakatalishi vikitumika na vinuruweo huwa na umuhimu gani katika kufundisha na kujifunza sarufi? Weka kikwaju (√) iwapo unakubali

| Kiwango | Nakubali | Nakataa |
|---|---|---|
| Hurahisisha uelewekaji wa sarufi | ✓ | |
| Husaidia kumbukumbu | ✓ | |
| Huchangia ubunifu. | ✓ | |
| Huendeleza vipawa | ✓ | |
| Huboresha matokeo ya ufundishaji | ✓ | |
| Huleta uvutio na kuboresha somo | ✓ | |

9. Wewe kama mwalimu wa sarufi, ni changamoto zipi hukukumba unapotumia vifaa vya kisasa vya ufundishaji?

- Ukosefu wa muda wa matayarisho
- Hitilafu za mara kwa mara za Umeme.
- Idadi kubwa ya wanafunzi
- ~~Sina~~ Hakuna Mtandao shuleni.

## KIAMBATISHO B: HOJAJI KWA MWANAFUNZI

KIAMBATISHO B: HOJAJI KWA MWANAFUNZI

Mimi ni Melly Kipchirchir Joachim,mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha kibabii.Nimetayarisha hojaji hii kutafiti kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji wa sarufi katika shule za upili. Nakuomba utenge muda wa kujibu maswali ya hojaji hii.Ninaahidi kwamba habari zote utakazotoa zitahifadhiwa kwa siri wakati na baada ya utafiti huu.. Weka kikwaju (√) katika visanduku.

1. Wewe kama mwanafunzi unatumia tarakilishi katika shughuli zipi?

| | |
|---|---|
| Kufanya utafiti wa masomo | ✓ |
| Kuhifadhi nukuu | X |
| Kutazama mchezo wa kandanda | X |
| Kucheza mchezo wa kamari | X |
| Kutazama filamu | ✓ |
| Kuwasiliana na marafiki mtandaoni | X |
| Kuhifadhi na kutazama muziki | X |
| Kutafuta maswali ya marudio mtandaoni | ✓ |

Iwapo una matumizi zaidi taja……………………………………………

……1) Kufanya uchambuzi wa Vitabu……………………………………

……2) Kutazama ~~na~~ mott uigizaji na michezo ya Vitabu……………………

……3) Kutazama filamu zenye mafundisho……………………………

……………………………………………………………………………

2. Unatumia kipakatalishi kinapounganishwa na kinuruweo kufanya nini?

| | |
|---|---|
| Shughuli za masomo | ✓ |
| Kurusha filamu nyakati za matumbuizo | ✗ |

Je, una matumizi zaidi? Iwapo yapo, yaorodheshe……………………………………

…Sina………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……….

……………………………………………………………………………………………

…

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……….

3. Kwa maoni yako, matumizi haya ya tarakilishi na vipakatalishi yana umuhimu gani?...i) Hurahisisha uelewekaji…………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

4. Ni changamoto zipi hukumba matumizi haya?……………………………………

…ii) Hatuna muda wa kutumia………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

7

## KIAMBATISHO C: MWONGOZO WA UCHUNZAJI WA AINA MBALIMBALI ZA VIFAA VYA KISASA VINAVYOPATIKANA SHULENI

KIAMBATISHO C: MWONGOZO WA UCHUNZAJI WA AINA MBALIMBALI ZA

VIFAA VYA KISASA VINAVYOPATIKANA SHULENI

| Aina ya vifaa | Vinapatikana kwa wingi | Vinapatikana wastani | Havipatikani |
|---|---|---|---|
| Majarida | | ✓ | |
| Magazeti | ✓ | | |
| Tarakilishi | | ✓ | |
| Filamu | | | ✓ |
| Projekta | | ✓ | |
| Runinga | | | |
| Redio | | | ✓ |
| Kanda za video | | | ✓ |
| Vinanda | | | ✓ |
| Tepu rekoda | | | ✓ |
| Vipakatalishi | | ✓ | |
| Chati | ✓ | | |
| Vitabu vya kiada | ✓ | | |
| Vitabu vya ziada | ✓ | | |
| Grafu | ✓ | | |

8

## KIAMBATISHO D: MWONGOZO WA UCHUNZAJI WA UFUNDISHAJI WA SOMO LA SARUFI

KIAMBATISHO D: MWONGOZO WA UCHUNZAJI WA UFUNDISHAJI WA SOMO LA SARUFI

1. Vifaa anavyotumia mwalimu katika somo — Mkwaju (√)

| | |
|---|---|
| Majarida | |
| Magazeti | |
| Filamu | |
| Redio | |
| Kanda za video | |
| Tarakilishi | |
| Tepu | |
| Kinuruweo | |
| Ubao | √ |
| Chaki | √ |
| Kipakatalishi | |
| Chati | |
| Grafu | |
| Ensaikolopidia | |
| Vitabu vya kiada | √ |
| Vitabu vya ziada | |

## KIAMBATISHO E: MWONGOZO WA MAHOJIANO KWA WALIMU

1. Wewe kama mwalimu wa Kiswahili, unatumiaje tarakilishi kufundisha mada za sarufi zifuatazo?

a) Usemi halisi na usemi wa taarifa

b) Muundo wa sentensi

c) Uakifishaji

d) Nyakati na hali

e) Vielezi

2. Unatumiaje vipakatalishi vinapounganishwa na vinuruweo kufundisha mada za sarufi zifuatazo?

a) Usemi halisi na usemi wa taarifa

b) Muundo wa sentensi

c) Uakifishaji

d) Nyakati na hali

e) Vielezi

f) Uchanganuzi wa sentensi

3. Kutokana na matumizi haya, vifaa hivi vina umuhimu gani katika ufundishaji wa sarufi?

4. Ni changamoto zipi hukumba matumizi haya ya tarakilishi na vipakatalishi vinapotumika na vinuruweo?

**KIAMBATISHO F: SHULE ZILIZOHUSISHWA KATIKA UTAFITI**

1. Shule ya Sekondari ya Kuinet.

2. Shule ya Sekondari ya Itigo.

3. Shule ya Sekondari ya Chuo kikuu cha Eldoret.

4. Shule ya Wasichana ya Moi

5. Shule ya Sekondari ya Eldoret ya Kati

6. Shule ya Sekondari ya Kimumu


7. Shule ya Wasichana ya Seko.

8. Shule ya Sekondari ya Eldoret G.K Magereza

## KIAMBATISHO H: MFANO WA CHUMBA CHA TEHAMA



## KIAMBATISHO I: RAMANI YA KAUNTI NDOGO YA MOIBEN



## KIAMBATISHO J: BARUA YA UTAFITI KUTOKA KIBABII

**KIBABII UNIVERSITY**
*(Knowledge for Development)*

Tel: 020 – 2028660 / 0708 – 085934 / 0734 - 831729
P.O. Box 1699 – 50200
Bungoma
Kenya

E-mail: enquiries@kibabiiuniversity.ac.ke / registrar.adm58@yahoo.com
Website: http://www.kibu.ac.ke

**OFFICE OF THE DEAN**
*SCHOOL OF GRADUATE STUDIES*

**Ref**: KIBU/SGS/CORR.033/VOL.1-2015/136

**Date:** 4th February 2019

Dear Melly Kipchirchir Joachim
Reg. No: MED/KIS/012/15

**RE: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

I am pleased to inform you that the Senate of Kibabii University acting on the advice of the Board of the School of Graduate Studies approved your proposal Entitled: **"Matumizi ya Vifaa vya Kisasa Katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi: Uchunguzi wa Shule za Sekondari Katika Kaunti Ndogo ya Moiben"** and appointed the following as supervisors:

1. Dr. Misiko Wasike
2. Dr. Edwin Masinde

You will be required to submit through your supervisor(s) progress reports every three months to the Dean SGS. Reports should be copied to the following: Chairman, FGSC-FESS and Chairman, DGSC-KOAL.

It is the policy of the University that you observe a deadline of two years from the date of registration for a Masters thesis. Do not hesitate to consult this office incase of any problem encountered in the course of your work.

Yours Sincerely,

Prof. S. N. Mutsotso
**Dean, SGS**

**Copy to:** Vice Chancellor
Deputy Vice Chancellor (ASA)
Deputy Vice Chancellor (AFD)
Deputy Vice Chancellor (PPRI)
Director PC&QA

**Kibabii University ISO 9001:2015 Certified**
**Knowledge for Development**

## KIAMBATISHO K: IDHINI YA UTAFITI KUTOKA NACOSTI

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. MELLY KIPCHIRCHIR JOACHIM***
**of KIBABII UNIVERSITY, 430-30300**
**KAPSABET,has been permitted to**
**conduct research in *Uasin-Gishu***
***County***

**on the topic: *MATUMIZI YA VIFAA VYA KISASA KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA SARUFI:UCHUNGUZI WA SHULE ZA SEKONDARI KATIKA KAUNTI NDOGO YA MOIBEN***

**for the period ending:**
***26th February,2020***

**Permit No : NACOSTI/P/19/62469/28365**
**Date Of Issue : 26th February,2019**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



..........................
***Applicant's Signature***

..........................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

## KIAMBATISHO L: IDHINI KUTOKA KAUNTI YA UASIN GISHU

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,**
**TION**

Telephone:
2241349,3310571,2219420
Fax: +254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref. No. **NACOSTI/P/19/62469/28365**

Date: **26th February, 2019**

COUNTY COMMISSIONER
UASIN GISHU COUNTY

Melly Kipchirchir Joachim
Kibabii University
P.O. Box 1699-50200
**BUNGOMA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on "***Matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi: Uchunguzi wa shule za sekondari katika Kaunti Ndogo ya Moiben***" I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Nairobi County** for the period ending **26th February, 2020.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Uasin Gishu County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Uasin Gishu County.

FOR COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
UASIN GISHU COUNTY
P. O. Box 9843, ELDORET

**KIAMBATISHO M: MFANO WA SLAIDI YA UAKIFISHAJI.**

